

**UPIMAJI WA KIWANGO CHA UELEWA WA MOFIMU ZA  
UAMBISHAJI NA UNYAMBULISHAJI WA KISWAHILI SANIFU KWA  
WANAFUNZI WA SEKONDARI TANZANIA**

**NDALAHWA BUNZALI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA  
MASHARTI YA MA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU HURIA CHA  
TANZANIA**

**2019**

## **UTHIBITISHO**

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu iitwayo *Upimaji Kiwango cha Uelewa wa Mofimu za Uambishaji na Unyambulishaji wa Kiswahili Sanifu kwa Wanafunzi wa Sekondari Tanzania* na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Dkt. Zelda Elsifa

(Msimamizi)

Tarehe.....

**HAKI MILIKI**

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile tасnifu hii, kwa njia ya kielektroniki, kurudufu au njia yoyote ile bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi.

**TAMKO**

Mimi, Ndalahwa Bunzali, nathibitisha kuwa tasnifu hii iitwayo *Upimaji Kiwango cha Uelewa wa Mofimu za Uambishaji na Unyambulishaji wa Kiswahili Sanifu kwa Wanafunzi wa Sekondari Tanzania* ni kazi yangu mwenyewe na kwamba haijawahi kufanywa na kuhudhurishwa na mtu mwengine yejote kwa lengo la kufuzu shahada ya umahiri katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

**Ndalahwa Bunzali**

.....

**Tarehe**

**TABARUKU**

Naitabarruku kazi hii kwa watoto wangu wapendwa, Shukurani Mitanga na Janneth Mitanga, ili iweze kuwatia hamasa ya kusoma zaidi ili nao Mungu akipenda waweze kufikia au kupita ngazi hii ya elimu.

## SHUKURANI

Awali ya yote natoa shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu, Muumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo, kwa kunijalia uzima, fikra na weledi wa kuandika mpaka kukamilisha kazi hii. Kwa hakika bila ya ye ye kunipa rehema zake lolote haliwezi kufanyika. Tasnifu hii imekamilika kutokana na msaada wa watu mbalimbali ambao wameweza kutoa mchango wao wa kihali, mali, mawazo na kifedha uliosaidia kufanikisha kazi hii yenye tija kwa wanafunzi wa sekondari.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaonesha kuguswa na mchango wa watu waliowezesha kukamilika kwa kazi hii. Ni vigumu kuwataja wote ila nawashukuru moyo mkunjufu kabisa kwa michango yao. Hata hivyo nitawataja wachache kwa niaba yao.

Shukurani zangu za pekee zimwendee msimamizi wangu, Dkt. Zelda Elisifa, kwa kujitoa kuisimamia kazi hii. Mungu azidi kumbariki, kumpa afya njema, hekima ili kazi zinazopitia mikononi mwake ziweze kuwa msaada mkubwa katika mstakabali wa taifa letu. Ninamshukuru kwa uvumilivu wake mkubwa tokea hatua ya kuandika pendekezo la utafiti hadi kumalizika kwa kazi hii. Kumalizika kwa kazi hii kumetokana na juhudhi yake kubwa ya kusoma, kukosoa, kurekebisha, kuelekeza na kushauri yale yote ambayo aliona yanafaa kuzingatiwa katika utafiti huu.

Shukurani za dhati pia zimwendee Dkt, Omary Mohamed kwa maelekezo yake ya awali ya namna ya kuandika pendekezo la utafiti. Sina cha kumlipa ila namuombea dua kwa Allah ampe maisha marefu na amzidishie nguvu na Imani ili aendelee kutoa mchango kwa wanataluma na taifa kwa ujumla.

Pia natoa shukurani nyingi kwa wahadhiri wangu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania wakiwakilishwa na Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Hanna Simpasa, Dkt. Nestory Ligembe na Prof.James Mdee. Namuomba Mungu awape maisha marefu yenye furaha na amani tele.

Nawashukuru pia wanafunzi wenzangu wote wa shahada ya uzamili ya Kiswahili wa mwaka wa masomo 2016/2017 hasa darasa la Mwanza, kwa ushirikiano wao mkubwa walionesha katika masuala ya taaluma kwa kipindi chote cha masomo ya umahiri. Vilevile nawashukuru kwa namna ya pekee familia yangu: mama yangu Mariamu Kanyasu, mke wangu mpendwa, Irene Shija Ngunda, mwanangu, Shukuru Mitanga, na binti yangu, Janneth Mitanga, pamoja na ndugu zangu wote wa familia kwa kunitia moyo na kuniendeleza kielimu hadi nimefikia ngazi hii ya juu. Mungu awabariki sana wote hao na aendelee kuwatunza kiafya, kimwili na kiroho.

## **IKISIRI**

Utafiti huu ulipima kiwango cha uelewa wa mofimu za uambishaji na unyambulishaji wa mofimu za maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania. Utafiti ulifanyika Mkoa wa Tabora wilaya za Uyui, Nzega na Manispaa. Mtafiti aliongozwa na malengo makuu mawili: Kubainisha kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu mofimu tangulizi, fuatishi na kubainisha sababu zinazosababisha wanafunzi wa sekondari kuwa na kiwango kitakachobainika kwenye lengo na. 1. Ili kufikia lengo kuu mbinu tatu za kukusanya data zimetumika: jaribio, dodoso na usaili. Utafiti uliongozwa na nadharia ya utambuzi. Utafiti ulibaini kuwa wanafunzi wanapokuwa kidato cha pili huonekana kama wameielewa mada ya mofimu lakini ufaulu wao hushuka kadiri wanavyopanda kidato cha tatu hadi cha nne. Kuthibitisha hilo, wanafunzi wa kidato cha tatu na nne walionekana kutofanya vizuri walipokuwa wanajibu maswali ya mofimu ikilinganishwa na wanafunzi wa kidato cha pili. Utafiti umebaini sababu zinazosababisha wanafunzi kuwa na uelewa mdogo wa mofimu kwa wanafunzi wa sekondari kuwa ni pamoja na matumizi ya mbinu ya mhadhara yasiyo shirikishi kwa mwanafunzi ambapo mwalimu huonekana anajua kila kitu, mbinu ya kukaririsha inayolenga ufaulu mzuri wakati wa mitihani bila kumjengea mwanafunzi stadi za maisha kwa kumshirikisha kwa vitendo, na wanafunzi kushindwa kuwianisha maarifa mapya waliyojifunza na maisha yao ya kila siku na vipindi vya Kiswahili kwenye ratiba ni vichache. Hivyo, inapendekezwa kuwa kuna haja ya kuziangalia upya mada zingine zinazofundishwa katika ngazi hii ya elimu kama zinaenda sanjari na wakati wa sasa.

## YALIYOMO

<b>UTHIBITISHO .....</b>	<b>i</b>
<b>HAKI MILIKI .....</b>	<b>ii</b>
<b>TAMKO .....</b>	<b>iii</b>
<b>TABARUKU .....</b>	<b>iv</b>
<b>SHUKURANI.....</b>	<b>v</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>vii</b>
<b>ORODHA YA MAJENDWALI.....</b>	<b>xii</b>
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
<b>1.0      UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
1.1     Usuli wa Tatizo la Utafiti .....	1
1.2     Tamko la Tatizo la Utafiti .....	3
1.3     Lengo Kuu la Utafiti .....	4
1.3.1     Malengo Mahsus ya Utafiti .....	5
1.3.2     Maswali ya Utafiti .....	5
1.4     Umuhimu wa Utafiti .....	5
1.5     Mawanda ya Utafiti .....	6
1.6     Changamoto za utafiti .....	6
1.7     Mpangilio wa Tasnifu .....	7
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>8</b>
<b>2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA .....</b>	<b>8</b>
2.1     Utangulizi .....	8
2.2     Mapitio ya Kitaaluma na Mapitio ya kazi tangulizi.....	8
2.3     Dhana ya Lughya,Lughya ya Asili, Lughya Mama na Lughya ya Pili.....	8
2.4     Dhana ya Upimaji katika Elimu na Isimu .....	10
2.5     Mapitio ya Kazi Tangulizi.....	10

2.6	Pengo la Utafiti.....	14
2.7	Mkabala wa Kinadharia .....	15
2.8	Hitimisho.....	16
	<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>17</b>
	<b>3.0 MBINU ZA UTAFITI .....</b>	<b>17</b>
3.1	Utangulizi.....	17
3.2	Usanifu wa Utafiti.....	17
3.3	Eneo la Utafiti .....	17
3.4	Kundi Lengwa .....	18
3.5	Sampuli na Usampulishaji wa Kundi Lengwa .....	18
3.6	Aina za Data Zilizokusanywa.....	21
3.6.1	Data za Msingi.....	21
3.7	Mbinu za Kukusanya Data .....	21
3.7.1	Mbinu ya Jaribio .....	21
3.7.2	Mapitio ya Insha .....	23
3.7.3.1	Insha za Ubunifu.....	23
3.7.3.2	Insha za Kiuamilifu.....	24
3.7.4	Dodoso .....	24
3.7.5	Mbinu ya Usaili .....	25
3 .8	Mbinu za Uchambuzi wa Data .....	27
3.9	Maadili ya Utafiti.....	27
3.10	Hitimisho.....	28
	<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>29</b>
	<b>4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI .....</b>	<b>29</b>
4.1	Utangulizi.....	29
4.2	Taarifa ya watafitiwa .....	29

4.2.1	Walimu wa Somo la Kiswahili.....	29
4.2.2	Idadi ya Wanafunzi.....	30
4.3	Kiwango cha Uelewa wa Wanafunzi Kuhusu Mofimu.....	31
4.4	Kiwango cha Uelewa wa Mofimu za Uambishaji na Unyambulishaji wa Maneno ya Kiswahili Sanifu.....	32
4.4.1	Uelewa kuhusu mofimu za mnyambuliko wa vitenzi .....	36
4.4.2	Kauli zinazotokana na unyambulishaji wa vitenzi vya maneno ya Kiswahili sanifu.....	38
4.4.3	Kanuni Zinazotumika katika Mnyambuliko wa Vitenzi vya Kiswahili Sanifu .....	42
4.5	Sababu Zinazofanya Wanafunzi kuwa na Uelewa Mdogo .....	44
4.5.1	Mbinu ya Kufundishia Inayotumiwa na Walimu wa Sekondari .....	45
4.5.2	Lugha ya Kiingereza Kuendelea Kutumika Kufundishia na Kutumika katika Mawasiliano ya Kawaida .....	47
4.5.3	Wanafunzi kutokuwa na muda wa kujisomea .....	50
4.5.4	Upungufu kwenye Mtaala wa Somo la Kiswahili .....	51
4.5.5	Mapungufu ya Muhitasari wa Kiswahili Sekondari .....	55
4.5.6	Maoni kuhusu Kiwango cha Uelewa wa Mofimu wa Wanafunzi .....	57
4.6	Hitimisho.....	59
<b>SURA YA TANO</b>	<b>.....</b>	<b>61</b>
<b>5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO</b>	<b>.....</b>	<b>61</b>
5.1	Utangulizi.....	61
5.2	Muhtasari .....	61
5.2.1	Muhtasari wa Ujumla .....	61
5.2.2	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	62
5.3	Hitimisho .....	64
5.4	Mapendekezo .....	65

5.4.1	Mapendekezo ya Kiutekelezaji.....	65
5.4.2	Mapendekezo ya Tafiti Fuatishi .....	65
<b>MAREJEREO.....</b>	<b>67</b>	

## **ORODHA YA MAJENDWALI**

Jedwali Na 3.1: Mgawanyo wa Sampuli .....	20
Jedwali Na.4.1: Ujazaji wa hojaji Kiidadi na kwa Asilimia .....	30
Jedwali Na. 4.2: Idadi ya wanafunzi watafitiwa sekondari kwa jinsi zao .....	31
Jedwali Na.4.4: Uelewa wa Wanafunzi Kuhusu Mofimu Za Uambishaji .....	34
Jedwali Na.4.5: Viambishi vya unyambulishaji.....	37
Jedwali Na. 4.6: Uelewa wa mofimu za utendea katika mnyambuliko wa vitenzi .....	38
Jedwali Na.4.8: Mbinu za kufundishia na kujifunzia Wanazotumia Walimu.....	46
Jedwali Na.4.10: Lughya ya Kiingereza Kuendelea Kutumika kunaathiri Ujifunzaji wa Mofimu?.....	49
Jedwali Na.4.11: Wanafunzi kutokuwa na Muda wa Kujisomea wanapokuwa nyumbani ....	50
Jedwali Na: 4.12: Uwiano wa Mada ya Mofimu na Mada Zingine za Isimu .....	58

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

#### **1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Historia inaonesha kwamba istilahi ya mofimu imeanza kutumika mnamo karne ya 18. Kwa mujibu wa Crystal (1971), wakati wa sarufi mapokeo (SM) uchambuzi wa kiisimu uliishia kwenye neno. Neno ndilo lililokuwa kipashio kidogo zaidi cha uchambuzi wa kiisimu. Katika kipindi hiki sentensi iligawanywa katika vipashio vidogo vidogo kama vile vishazi, virai na hatimaye neno (N) lakini baadaye katika karne za 18 na 19 ilibainika kuwa palikuwa na haja ya kwenda chini zaidi ya neno. Wakati huu ndipo isitlahi ya mofimu ilipoanza kutumika. Kauli hii ya uchanga wa mofimu inakuja kudhihirishwa na wataalamu mbalimbali, kwa mfano Mugullu (1999) anapobainisha sura kuu mbili za dhana ya mofimu zinazotofautiana sana. Sura hizo zinalingana na vipindi vikuu viwili ambamo dhana hii ilitumika, dhana ya mofimu kabla ya kuasiwi kwa sarufi zalishi (SZ) na dhana ya mofimu baada ya kuasiwi kwa sarufi zalishi katika karne ya 20.

Tunapochunguza mofimu za lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili, wataalam mbalimali wamejadili mada hii. Mfano Masebo na Nyangwine (2007) wanaeleza kuwa, lugha ya pili ni lugha ambayo binadamu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza. Kiswahili ni lugha ya pili kwa watu wengi wa Tanzania. Kujifunza lugha ya pili kunatawaliwa na vitu mbalimbali kama vile walimu wanaofundisha na vifaa vya kufundishia. Pamoja na maelezo yaliyotolewa na Masebo na Nyangwine (wameishatajwa) kuhusu vitu vinavyotawala ujifunzaji wa lugha, jamii

inayomzunguka anayejifunza lugha huutawala pia. Kwa mfano mtu anayejifunza Kiswahili akiwa Tanzania na anayejifunza Kiswahili akiwa Zimbabwe, Ghana au Ureno, atakayekifahamu Kiswahili mapema ni yule ajifunzaye Kiswahili hicho akiwa Tanzania. Tofauti kati ya mifumo-sauti ya lugha zinadhihirika zaidi wakati mtu anapojifunza lugha ya pili baada ya kuwa amekwishajua lugha yake ya mwanzo. Wakati huo, mfumo-sauti wa lugha yake umekwishaimarika kwa kiasi kikubwa na akijifunza lugha ya pili, mara nyingi anatafasiri sauti za lugha hii mpya kwa misingi ya fonolojia ya lugha yake ya kwanza. Lugha ya pili hutumika katika kukidhi haja za mawasiliano na jamii ambazo siyo lugha yake ya kwanza. Hivyo kujifunza ni kwa lazima kwa lengo la mawasiliano na pia kujihusisha na jamii inayozungumza lugha hiyo.

Uchunguzi wa ujifunzaji wa lugha za Kiafrika na hasa katika mukutadha wa matumizi yake kama lugha za kufundishia kwa kiasi kikubwa zimefanywa ndani na nje ya Tanzania. Hata hivyo ipo mifano michache ya tafiti hizi hapa Tanzania; kwa mfano, Mashaka (2015) alijishughulisha na athari za lugha ya Kijita katika kujifunza Kiswahili na kuona kwamba kila lugha ina misingi na kanuni zake katika utamkaji na uundaji wa maneno mfano, katika lugha ya Kijita sauti [dh], haipo badala yake hutumia sauti ya [z]. Hii inadhihirisha kuwa kila lugha hutawaliwa na kanuni zake. Hivyo basi, kanuni ya pekee ya lugha ya Kiswahili ni kuwa na uwezo wa neno kujitosheleza na kujieleza lenyewe bila ya msaada wa maneno mengine. Kujitosheleza kwa neno la Kiswahili ni kutokana na kunyambulika kwake.

Mada yetu ni upimaji wa kiwango cha uelewa wa mofimu na aina zake kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania. Upimaji katika elimu ni tendo la kutafuta ni kwa kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa au stadi zilizofundishwa kufuatana na malengo ya ufundishaji wa mada za somo zilizopo kwenye muhtasari. Upimaji humuonesha anayejifunza ni mahali gani ana mapungufu na humfanya anayefundisha ajue ni mahali gani amefanikiwa na ni wapi hajafanikiwa.

## **1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti**

Lugha ya kufundishia ni lugha inayopaswa kufahamika kwa kiwango kukubwa kwa wanaoifahamu. Kimsingi lugha hiyo hupendekezwa iwe na hadhi ya lugha ya kwanza (L1) kwa wanaoitumia kama Kiingereza kwa Waingereza na Wamarekani, Kijerumani kwa Wajerumani, Kijapani kwa Wajapani, nk. Hata hivyo kuna mazingira yanayoruhusu lugha ya pili (L2) katika muktadha wa isimujamii kutumika kama lugha ya kufundishia ili mradi wote wanoitumia kama lugha ya kujifunzia wana ubobezi nayo wa kutosha. Hivi ndivyo ilivyo kwa Kiswahili Tanzania.

Hata hivyo kumekuwa na malalamiko mengi ya walimu wanaofundisha somo hili, kuwa Kiswahili hakifamamiki kwa wote na hasa katika nyanja ya isimu. Mojawapo ya mada inayoonekana kutokuwa na ufahamu wa kutosha ni ya mofimu. Mada hii huanza kufundishwa kuanzia kidato cha pili kama ilivyo kwenye muhutasari wa Kiswahili sekondari. Kwa mfano muhutasari wa matokeo ya kidato cha pili wa mwaka 2015 unaonesha kuwa wanafunzi wanapokuwa kidato cha pili ufaulu wao unakuwa wa wastani tofauti na wanapokuwa kidato cha nne kama taarifa ya Baraza la Mitihani la Taifa inavyojieleza. Jambo hili pia linathibitishwa na taarifa ya watahini kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa kuhitim

kidato cha nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2014 na 2015 ambapo mtihani wa mwaka 2014 sehemu (A) ilihu mofimu za utendea, mwaka 2015 sehemu (B) ilihu matumizi ya mofimu (NECTA, 2014, 2015).

Pia mada za ubobezi wa lugha ya kufundishia na kujifunzia zimewahi kufanyiwa tafiti nyingi za kielimu kama vile tafiti zilizofanywa na Rubagumya (1996, 1999), Qorro (1997), Kiputiputi (2001), Msanjila (1988, 2005) na TUKI (2003, 2004) zilihusu hali ya Kiswahili katika shule za sekondari Tanzania. Utafiti uliofanywa na HakiElimu (2014) unaonesha kuwa viwango vya ufaulu wa somo la Kiswahili uko chini ukilinganisha na masomo mengine yanayofundishwa sekondari kama vile Hisabati, Kiingereza na masomo mengine katika wilaya zilizochaguliwa.

Hata hivyo maswali yanaibuka : ufaulu huu dhaifu ni kwa kiwango gani? Je inakuwaje mada ifundishwe kidato cha pili na wanafunzi waoneshe ufahamu mzuri lakini wanapofika kidato cha nne ufaulu huu ushuke ? Pia licha ya tafiti hapo juu zinazohusiana na ufundishaji na ujifunzaji wa mada za Kiswahili, hakuna utafiti unaopima uelewa wa wanafunzi wa sekondari Tanzania kuhusu mada ya mofimu. Ni katika ombwe hilo utafiti huu ulipima kiwango cha uelewa wa mofimu tangulizi kwa aina zake, mofimu fuatishi kwa aina zake kwa wanafunzi wa sekondari.

### **1.3 Lengo Kuu la Utafiti**

Kupima kiwango cha uelewa wa mofimu za uambishaji na unyambulishaji wa maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania.

### **1.3.1 Malengo Mahsusini ya Utafiti**

1. Kubaini kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu mofimu tangulizi na mofimu fuatishi katika vitenzi vya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania
2. Kubainisha sababu zinasababisha wanafunzi wa sekondari kuwa na kiwango kitakachobainika kwenye lengo na. 1

### **1.3.2 Maswali ya Utafiti**

1. Ni kipi kiwango cha uelewa wa mofimu tangulizi na mofimu fuatishikatika vitenzi vya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania?
2. Ni sababu gani zinazosababisha uelewa wa mofimu za uambishaji wa maneno ya Kiswahili sanifu utakaodhahirika kwenye swali namba moja?

## **1.4 Umuhimu wa Utafiti**

Umuhimu wa utafiti huu ulijikita katika nyanja kuu tatu:

Kwanza, utafiti huu unategemewa kutoa mchango katika kuboresha mtaala wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari nchini na hivyo kufanya kuwa na muhtasari unaota matunda kwa wanafunzi na hivyo kuwafanya waweze kumudu mada za isimu kwenye ngazi zinazofuata za kielimu.

Pili, utafiti huu unategemewa kuwawezesha wanafunzi na walimu kuongeza uelewa na kubaini mbinu mbalimbali zinazotumika katika suala zima la ujifunzaji na ufundishaji wa mofimu na aina zake, viambishi awali na viambishi tamati kwa aina zake, aina za mizizi, aina za mashina, matumizi ya mofimu,

mnyambuliko wa maneno katika vitenzi,dhana ya uambishaji na dhana ya unyambulishaji. Tatu, utafiti huu utakuwa chachu kwa watafiti wengine kufanya tafiti zaidi katika mtaala wa elimu hususani katika mada za isimu zilizomo sasa na ambazo hazijawekwa kwenye silabasi ya Kiswahili sekondari na hivyo utatumika kama marejeo kwa watafiti wengine.

### **1.5 Mawanda ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita kwenye kubaini kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu mofimu tangulizi na mofimu fuatishi katika vitenzi vyta Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania na kubainisha sababu zinasababisha wanafunzi wa sekondari kuwa na kiwango kitakachobainika kwenye lengo na. 1

Pia kundi lengwa ni wanafunzi wa sekondari za Upuge, Puge, Uyui, Idete, Manoleo na Imalampaka. Hata hivyo ni baadhi tu ya mikondo ya madarasa ndio iliyohusishwa katika utafiti huu. Pamoja na hayo sio kila kidato kilihusishwa katika utafiti huu, bali walihusishwa wanafunzi wa kidato cha pili, tatu na cha nne kwa kuwa ndio wanaojifunza mada ya mofimu.

### **1.6 Changamoto za utafiti**

Utafiti huu ulikabiliwa na changamoto moja, kama ifuatavyo.

Matumizi ya dodoso yalikuwa na hatari ya kuwapa mwanya watafitiwa kuingiza hisia zao wenywewe ambazo zisingeweza kuwa na ubora wa data tarajiwa. Hata hivyo changamoto hii ilitatuliwa kwa kuwa na mbinu nyingine za kukusanya data zaidi ya mbinu hii ya dodoso.

### **1.7 Mpangilio wa Tasnifu**

Tasnifu hii ina jumla ya sura kuu tano zenyenye mada kuu na mada ndogondogo ndani yake. Sura ya kwanza ina vipengele mbalimbali vyatia kiutangulizi. Vipengele hivyo ni Usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, lengo la jumla la utafiti, malengo mahususi ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu. Sura ya pili ambayo imeelezea mapitio ya kazi tangulizi ambazo zimefanywa na watafiti mbalimbali kuhusu mada yetu. Sura ya tatu imewasilisha sampuli, usampulishaji, mbinu za kukusanya data za utafiti. Sura ya nne imehudhurisha uchambuzi wa data za utafiti na sura ya tano imetoa muhutasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## **SURA YA PILI**

### **2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii inawasilisha mapitio ya kitaaluma ya kinadharia naya tafiti tangulizi. Marejeleo ya vitabu na Machapisho yanayohusiana na mada ya utafiti huu yamehusika. Sura hii imeangalia kazi za wataalamu waliofafiti upimaji wa uelewa wa lugha. Katika sehemu hii fasili ya lugha, lugha ya kwanza na lugha ya pili zimefanuliwa. Tumebainisha yaliyoandikwa kuhusu mada ya mofimu na upimaji wa uelewa katika lugha mbalimbali kisha katika lugha ya Kiswahili. Pia, pengo la utafiti na kiunzi cha nadharia vimeonyeshwa ndani ya sehemu hii.

#### **2.2 Mapitio ya Kitaaluma na Mapitio ya kazi tangulizi.**

Katika sehemu hii fasili ya lugha, lugha ya asili, lugha ya kwanza na lugha ya pili, uamiliaji lugha, ujifunzaji lugha na matumizi ya lugha ya pili, nadhana ya upimaji vimeelezewa. Kisha pengo la maarifa limeainishwa na kufuatiwa na kiunzi cha nadharia.

#### **2.3 Dhana ya Lugha,Lugha ya Asili, Lugha Mama na Lugha ya Pili**

Kabla ya kuongelea juu ya dhana ya upimaji katika elimu, ni jambo la muhimu kuelewa kwanza fasili ya lugha.Wataalam mbalimbali wameielezea lugha kwa namna zinazotofautiana.Wafuatao ni mionganini mwa wataalamu hao. Habwe na Karanja (2004), wakiinukuu TUKI (1990), wanasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu katika jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Massamba na wenzake (2009) wanaeleza kuwa lugha ni mfumo wa

sauti nasibu ambazo zimebuniwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao. Hivyo basi, kulingana na maelezo ya wataalam hao, lugha ni mfumo wa sauti nasibu ambazo hutumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana kwa madhumuni ya mawasiliano mionganoni mwa jamii hiyo.

Kwa upande wa lugha ya pili (L2), Masebo na Nyangwine (2008) wanasesma kuwa ni lugha ambayo binadamu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza. Kiswahili ni lugha ya pili kwa watu wengi wa Tanzania. Msanjila na wenzake wanaeleza kuwa lugha ya pili ni lugha anayojifunza mtu baada ya lugha yake ya kwanza au lugha mama. Kimsingi lugha ya pili huwa ni lugha rasmi inayotumiwa katika elimu, utawala na serikali. Kwa wazungumzaji wengine, lugha ya kwanza huwa pia ndio lugha ya pili kwa maana kwamba ndiyo lugha ya elimu, serikali na mawasiliano mapana.

Dhana ya ujifunzaji lugha, kwa mujibu wa Massamba (2004), ni utaratibu wa kufanya jitihada rasmi za kuijua na kuitumia lugha fulani. Mtu yejote ana uwezo wa kujifunza lugha na kuifahamu ikiwa tu atakuwa na akili timamu pamoja na alasauti zote zinazohusiana na ujifunzaji lugha, ilimradi ziwe hazijaathiriwa au kuathirika. Pamoja na maelezo yaliyotolewa na Masebo na Nyangwine (wameishatajwa) hapo juu kuhusu vitu vinavyotawala ujifunzaji wa lugha, jamii inayomzunguka anayejifunza lugha huutawala pia. Kwa mfano mtu anayejifunza Kiswahili akiwa hapa Tanzania na anayejifunza Kiswahili akiwa Zimbabwe, Ghana au Ureno, atakayekifahamu Kiswahili mapema ni yule ajifunzaye Kiswahili hicho akiwa Tanzania kwa kuwa atakuwa amechanganyikana na jamii inayotumia lugha hiyo katika mawasiliano.

## **2.4 Dhana ya Upimaji katika Elimu na Isimu**

Upimaji katika elimu ni tendo la kutafuta ni kwa kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa au stadi zilizofundishwa kufuatana na malengo ya ufundishaji wa mada za somo zilizo kwenye muhitasari. Upimaji katika elimu pia hujumuisha mwenendo na tabia ya mwanafunzi na uwezo wake wa kufanya mambo mbalimbali (Msanjira, 2005).

Dhana ya upimaji katika isimu ni tendo la kuchunguza ni kwa kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa juu ya kuchambua na kuchunguza lugha kwa kutumia misingi ya kisayansi katika matamshi, maumbo, miundo, maana na matumizi ya lugha. Upimaji katika isimu hautofautiani na ulivyo kwenye nyanja nyingine kama inavyoelezwa na Musumi (2016) aliposema kuwa katika elimu upimaji ni tendo la kutafuta ni kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa au stadi zilizofundishwa kufuatana na malengo ya ufundishaji wa mada za somo yaliyopo kwenye muhtasari. Upimaji katika elimu hujumuisha pia mwenendo na tabia ya mwanafunzi na uwezo wake wa kufanya mambo mbalimbali Mwalimu pia hupimwa kuonesha uwezo wake wa kufanikisha malengo ya elimu yaliyowekwa. Kigezo cha kupima mafanikio ya elimu ni malengo. Umuhimu wa upimaji katika elimu ni matokeo ya upimaji wa elimu hutumiwa na watu mbalimbali, kwa mfano, mwanafunzi, shule, wazazi, waajiri, walimu na watafiti (Msanjila, 2005).

## **2.5 Mapitio ya Kazi Tangulizi**

Mapitio ya kazi tangulizi tuliyoyaangalia hapa ni yale ambayo yana uhusiano na mada yetu ya utafiti, ambapo mjadala ulilenga kupima uelewa wa mofimu kwa

wanafunzi wa sekondari. Katika sehemu hii kuna maandiko yanayohusu mofimu za uambishaji na unyambuaji katika lugha ya Kiswahili sanifu. Achieng (2012) alichunguza uwezo na ujuzi wa stadi za Kiswahili katika shule za msingi nchini Kenya. Alieleza kuwa lugha ni kipengele muhimu sana katika maisha kwa kuwa hutumika kuelezea hisia na misukumo ya ndani. Alilinganisha lugha ya Kiluo (lugha mama) na Kiswahili zinavyorahisisha mawasiliano kwa kutumia stadi za kuandika, kuhesabu, kuzungumza na kusoma.

Kibuni (2012:26-31) alichunguza stadi za kusoma ufahamu na msamiati wa Kiingereza kwa wanafunzi wa Kenya kama lugha ya pili na kuibua changamoto zinazosababisha kuwa na uelewa mdogo katika maeneo ya ufahamu na msamiati. Anasema, kwamba kutohana na utafiti alioufanya aligundua kuna haja ya kuingilia kati mipango ya ufundishaji wa stadi ya kusoma ufahamu. Anasema tunahitaji kujenga na kuweka bayana misamiati inayopatikana katika makala, maudhui, muziki na mitindo ya uandishi. Neno uchambuzi lazima lifundishwe pia stadi ya kusoma lazima ilenge katika kuleta maendeleo katika suala zima la upokeaji na kutafsiri (TY). Kombo (2015) alichunguza umahiri wa lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wa Tanzania katika shule za msingi na sekondari. Alishughulikia uundaji wa sentensi zilizokamilika na zenyе maana. Aligundua kuwa wanafunzi wengi hawakufanya vizuri kwenye majaribio yaliyohusu stadi ya kusoma na kuandika.

Utafiti wa Uwezo (2011) ulionesha kuwa wanafunzi wengi wa shule za msingi za umma za Tanzania hawakuwa na uelewa wa kutosha katika lugha ya Kiingereza hususani kwenye stadi ya kusoma. Uchunguzi wao ulionesha kuwa asilimia 50 ya

wanafunzi wa darasa la VII hawakuwa wanaweza kusoma vitabu vyatia Kiingereza vya darasa la II.

Vuzo (2002) alitafiti sababu za kiwango kidogo cha ufaulu wa somo la Kiingereza kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania na aligundua kuwa asilimia kubwa ya wanafunzi walikuwa na uwezo mdogo katika umahiri wa kuandika. Msanjila (2005) alitathmini matatizo ya uandishi katika lugha ya Kiswahili. Katika utafiti wake alitofautisha kati ya stadi ya kuandika na ya kuzungumza. Aidha alibaini kuwa uandishi unaotumika katika kujibu maswali yasiyo fungo (huru) katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa sekondari za Tanzania bado una upungufu mkubwa na kupendekeza kuwa kuna haja ya kukazia stadi ya kuandika kwa kutumia maswali ya kujieleza kwani wanafunzi wengi bado hawakuweza kutofautisha kati ya kuandika kama kazi na kuandika kama ujuzi/umahiri. Msanjila anaendelea kusema kuwa matatizo mengi yanayojitokeza katika uandishi na makosa ya kisarufi yalisababishwa na uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia pia ufundishaji usiokidhi unaofanywa na walimu wa Kiswahili. Matatizo haya ya uandishi yalibainika kwa wanafunzi walipokuwa wanaandika insha walizopewa, Insha zilizowataka kubainisha matumizi ya mofimu za njeo, hali, ngeli, aina za viambishi na mofimu za utendea katika hotuba, pia wanafunzi walitakiwa sentensi kwa kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali.

Macdonald (1990) alibaini kuwa uelewa mdogo wa walimu katika lugha ya kufundishia nchini Botswana unawakosesha wanafunzi kufahamu maarifa yaliyotarajiwa kufikiwa na pia walimu hushindwa kuchagua mbinu sahihi na nzuri za kufundishia katika mada husika. Macdonald anaendelea kusema kuwa mwalimu wa

somo asipokuwa na umahiri wa mada anayokwenda kuiambukiza kwa wanafunzi ni dhahiri wanafunzi hao hawatapata maarifa yaliyotarajiwa wayapate. Makewa na wenzake (2013) katika kazi yao ya kupima kiwango cha uelewa wa lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari za Dodoma nchini Tanzania, wanasema kuwa kujifunza lugha ni mchakato wa kujifunza lugha ya pili baada ya kujifunza lugha ya kwanza. Hivyo kuna mambo mbalimbali yanayokwamisha ujifunzaji wa lugha ya pili (TY).

Baadhi ya mambo hayo yameelezwa kwa kirefu kwenye utafiti na uchanganuzi wa hoja uliofanywa na wataalamu mbalimbali umeendelea kudhihirisha matatizo ya kuendelea kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia, hasa elimu ya seondari. Miongoni mwa wataalamu hao ni Roy-Campbell na Qorro (1987), Qorro (1996), Yahya-Othman na Batibo (1996) na Simonds na wenzake (1996). Katika utafiti, makala na machapisho yao mengi wataalamu hao, na watafiti wengine wengi wamehoji na kudhihirisha pasi na mashaka kuwa: (i) hivi sasa Kiingereza hakitumiki tena ipasavyo kama lugha ya kufundishia; na hivyo (ii) kuendelea kutumia kiingereza kama lugha ya kufundishia elimu ya juu kunakwamisha uwasilishaji na upokeaji wa maarifa yaliyokusudiwa wanafunzi wayapate, (iii) kuendelea kutumia Kiingereza kunadumaza miongoni mwa wanafunzi weledi wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kadhalika kama lugha za mawasiliano ya kitaaluma, (iv) kuendelea kutumia Kiingereza katika hali kama hiyo kunaondoa uwezekano wa kufundisha vizuri Kiingereza, (v) kwa sababu ya tofauti baina ya lugha ya kufundishia masomo ya elimu ya juu na lugha ya mawasiliano ya kawaida haiyumkiniki tena kukiwezesha Kiingereza kutumika ipasavyo kama lugha ya kufundishia na (vi) hakuna shaka,

miongoni mwa wanataaluma mbali mbali, kuwa Kiswahili hata kwa hali yake ya sasa, kinafaa na kinaweza kutumika ipasavyo kufundishia masomo ya elimu ya juu. Walimu walithibitisha hili walipokua wanajibu maswali ya liyoulizwa na mtafiti kwa njia ya usaili na walipokuwa wanajibu swali namba sita lililowataka kutaja matatizo yaliyomo katika mtaala wa Kiswahili sekondari.

Rubagumya (1990) alipokuwa anashughulika na hali ya Kiswahili kutumika kufundishia elimu ya sekondari alisema kuwa, Kiswahili kinatakiwa kuwa chaguo la elimu ya sekondari kufundishia na mawasiliano na Kiingereza kibaki kama somo.

Shadrack (2016) alitafiti kutambua aina ya makosa ya kifonolojia na ya kimofolojia yanayodhihirika kwenye insha za wanafunzi wa kidato cha pili wanapojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Aligundua kuwa wanafunzi wa Kimeru wanatia nazali kabla ya konsonanti ya vipasuo ghuna /d/, /g/, na /b/. Hii ilijitokeza takribani kwenye insha zote zilizoandikwa na wanafunzi, ambapo ilidhihirisha kuwa lugha ya Kimeru ina mfumo tofauti na lugha ya kiswahili.

## **2.6 Pengo la Utafiti**

Kimsingi kuna tafiti nyingi za isimu ambazo zimefanywa za kuchunguza kiwango cha uelewa kwenye kipengele cha sarufi kwa wanafunzi wa sekondari. Hata hivyo, hakuna tafiti zilizofanywa kupima uelewa wa mofimu za Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Hivyo basi, ili kuziba pengo hilo utafiti huu umelenga kuongeza mchango huo kwa kupima kiwango cha uelewa wa mofimu za uambishaji na unyambulishaji wa maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari.

## 2.7 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ambayo tumeitumia katika kazi hii kama mwongozo wetu ni nadharia ya utambuzi. Miaka 50 iliyopita, Benjamin Bloom na wenzake waliainisha nyanja mbalimbali za utambuzi, mojawapo ya nyanja hizo ni hii ya utambuzi. Nadharia ya utambuzi inaonesha wazi kuwa wajifunzaji hujijengea maarifa wenye we wanapojifunza mmoja mmoja na wawapo kwenye vikundi vyao vya ujifunzaji na pia humfanya ajenge maana anapojifunza. Kuna matokeo mawili ya huu mtazamo. Kwanza, ni lazima mwalimu amfikirie mjifunzaji kwa mtazamo wa ujifunzaji na sio somo analokwenda kufundisha. Pili, hakuna maarifa yasiyohusiana na maana iliyojengwa kutokana na uzoefu wa wanafunzi au jamii ya wanaojifunza (Hein, 1991).

Nadharia hii inazo kanuni kadhaa zilizo tuongoza kupima kiwango cha uelewa wa mofimu za uambishaji na unyambulishaji wa maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari kwa shule zilizoteuliwa. Kanuni hizo zinazoongoza nadharia ya utambuzi ni hizi zifuatazo:-

Ujifunzaji ni mchakato husishi ambapo mjifunzaji anatumia anachokipokea akilini ili kujenga maana. Kanuni hii tuliiutmia wakati wa kuchambua insha zilizokuwa zimeandikwa na wanafunzi, ililazimika wakati mwangi kutumia njia ya majadiliano wakati wa kuwasilisha insha hizo. Watu hulazimika kujifunza wanapokuwa kwenye mchakato wa kujifunza: ujifunzaji unahusika kujenga maana kutokana na maarifa mapya ambayo mtu hujihusisha nayo. Nadharia hii tuliiutmia sana wakati wa kusahihisha majoribio yaliyotolewa kwa wanafunzi ambayo yalikuwa ya kuainisha njeo, kubaini aina ya viambishi vinavyoambishwa kwenye mizizi ya maneno ya

Kiswahili na pia kubainisha alomofu za utendea katika minyambuliko ya vitenzi. Kitendo hiki muhimu cha kujenga maana ni cha kiakili, kinatokea akilini, na pia cha kijamii kupitia kwenye mahusiano yetu na walimu wetu, rika zetu, jamii zetu na watu tunaofahamiana nao. Walimu wanapaswa kutoa mazoezi yanayohusisha akili, kama vile mazoezi ya tafakuri ambayo wanafunzi wanaweza kuyafanya peke yao, na mazoezi yanayohusisha mwili na kujenga mahusiano. Tulipokuwa tunachambua aina ya mazoezi, majoribio na mitihani ambayo walimu wamekuwa wakiitoa hapo shulen ikiwemo ya juma, kila mwezi na ya kufungia muhula; Kwa kutumia nadharia hii iliweza kutusaidia kugundua uelewa mdogo walionao wanafunzi kuhusu mada ya mofimu. Ujifunzaji unahuishisha lugha, na hivyo basi, lugha tunayoitumia madarasani na shulen kwa ujumla inaathiri ujifunzaji. Kadiri wanafunzi wanavyoizoea lugha inayotumika shulen, ndivyo wanavyoweza kushirikiana na kujenga maana kutokana na maarifa mapya. Ujifunzaji umekaa kimazingira. Tunajifunza kulingana na maarifa ya awali tuliyonayo (rasmi na yasiyo rasmi), tunachokiamini, upendeleo na hofu zetu (Hein 1991). Nadharia hii ilitusaidia wakati wa kupitia kazi za watafiti zilizohusu athari za lugha ya kwanza na mazingira yanavyochangia kumfanya mwanafunzi awe na uelewa mdogo wa matumizi ya njeo na hali katika ujifunzaji wa mofimu.

## **2.8 Hitimisho**

Katika sura hii tulitalii kazi anuwai kuhusu ujifunzaji wa lugha, haswa lugha ya pili (L2) na ya kufundishia. Pia tumeonesha ombwe la maarifa lililoachwa na tafiti hizo. Hatimaye tulionesha na kufafanua kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti.

## **SURA YA TATU**

### **3.0 MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Katika sura hii tumefafanua mbinu mbalimbali ambazo tulizitumia katika mchakato wa utafiti huu ili kuwezesha upatikanaji, uchambuaji na uwasilishaji wa data. Sura hii imebainisha eneo la utafiti na sababu za kuteua eneo hilo, usanifu wa utafiti, kundi lengwa kwa aina zake, usampulishaji, data zilizokusanywa, mbinu mbalimbali zilizotumika kukusanya data, mbinu za uchambuzi wa data, maadili ya utafiti na hitimisho ambalo limetoa muhitasari wa sura nzima.

#### **3.2 Usanifu wa Utafiti**

Utafiti kwa kawaida huweza kuwa na muundo wa kitakwimu ambao unajikita zaidi katika tafiti za kitakwimu na tafiti zinazohusika na data za kimaabara au muundo wa maelezo ambao unahusu zaidi tafiti za sayansi za kijamii ambapo kwa kawaida data zake zinachanganuliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia zaidi maelezo (Ryanga, 2007). Utafiti huu ulihusisha aina zote mbili za miundo ya takwimu na maelezo kutegemea na aina ya data.

#### **3.3 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika katika wilaya tatu Nzega, Uyui na Manispaa ya Tabora zote za mkoa wa Tabora. Mkoa wa Tabora umegawanywa katika wilaya za kiutawala saba ambazo huunda wilaya nane za kielimu ambazo ni wilaya ya Sikonge, Urambo, Kariua, Uyui, Nzega mji, Nzega DC, Igunga na Manispaa. Sababu za kuteua eneo hilo ni kwamba, shule za sekondari nilizozifanyia utafiti ziko karibu, hivyo nilizifikia

kirahisi. Aidha mtafiti alikuwa akifuatilia ufaulu wa somo la Kiswahili katika shule hizi kwa muda mrefu hali iliyopelekea apate hamu ya kulifanyia utafiti suala hili katika shule hizo. Utafiti huu ulihusisha jumla ya shule sita za sekondari kutoka katika wilaya tatu kwa kuhusisha shule za mjini na za kijiji.

### **3.4 Kundi Lengwa**

Waliman (2011) anasema kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti, yaani watu, taasisi, vitu au matukio. Kwa ujumla kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kwamba kundi lengwa ni wanachama wote, kikundi, mtu mmoja anaviashiria ambavyo mtafiti amekusudia kuvihusisha katika utafiti wake. Katika utafiti huu kundi lengwa lilikuwa ni wanafunzi na walimu wanaofundisha somo la kiswahili kidato cha Pili mpaka cha nne katika shule za sekondari Idete, Upuge, Imalampaka zote za serikali kutoka wilaya ya Uyui, Shule ya sekondari Puge kutoka wilaya ya Nzega shule ya serikali na shule mbili kutoka Manispaa ya Tabora ambazo ni Manoleo ni shule ya serikali na sekondari ya Uyui ambayo ni shule ya binafsi. Jumla ya walengwa walikuwa ni wanafunzi 90 na walimu 06 kutoka kwenye shule zote sita tulizozifanyia utafiti. Walengwa hawa walichaguliwa kwa kuwa ndio wenye uwezo wa kutoa taarifa tulizo zihitaji ili kukamilisha utafiti wetu.

### **3.5 Sampuli na Usampulishaji wa Kundi Lengwa**

Kothari (2004) amefafanua kuwa sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo kwalo mtafiti hupata data na

kutoa mahitimisho yake. Enon (199) anaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu kutoka kundi lengwa zima. Usampulishaji ulitumia mbinu za nasibu na usampulishaji lengwa. Usampulishaji nasibu, kama unavyofasiliwa na Ruane (2005) ni mchakato wa kuchagua sampuli ambapo uwezekano wa kuchagua mtafitiwa yejote katika kundi huwa na fursa sawa kuchaguliwa kuwa sehemu ya sampuli.

Kothari (2013) anasema mbinu ya usampulishaji nasibu au uteuzi rahisi ni mbinu inayotumika kuteua sampuli ya wahojiwa mionganoni mwa kundi kubwa la wahojiwa wenye sifa sawa. Sampuli katika mbinu hii huteuliwa kuwakilisha kundi kubwa bila kujali sifa ya mteuliwa kwani kila mmoja katika kundi hilo huwa na sifa sawa au zinazofanana yaani kuwa na wanafunzi wa sekondari wanaosoma somo la Kiswahili shuleni hapo. Tuliteuwa sampuli kwa kuchukua orodha ya majina ya wanafunzi. Kwa kutumia orodha hiyo tuliteua sampuli kwa kutumia nafasi ya kwanza kila baada ya mtu wa tatu. Aidha tulifanya hivyo pia kwa kuchagua majina ya wavulana na ya wasichana ili kupata idadi ya watafitiwa kwa kuzingatia jinsi. Uteuzi huu ulizingatia jinsi ili kuhakikisha jinsi zote zinashiriki katika utafiti huo.

Uteuzi huu wa sampuli wa kujali jinsi ulitumika pia tulipokuwa tunateua walimu katika shule sita lengwa ambapo ilizingatia hali ya ikama ya walimu wa Kiswahili katika shule husika. Njia ya pili tuliyotumia ni usampulishaji lengwa. Mbinu hii hutumika sanjari na mbinu nasibu. Tuliteua kundi lengwa amba ni kidato cha pili tatu na nne, kisha kutokana na idadi ya mikondo waliyokuwa nayo njia ya usampulishaji nasibu ilitumika kupata watafitiwa kutoka kila kidato kwa kila mkondo. Jedwali na.3.1 hapa chini linawasilisha mgawanyo wa sampuli.

### **Jedwali Na 3.1: Mgawanyo wa Sampuli**

<b>WALENGWA</b>	<b>JUMLA</b>	<b>WALIOSHIRIKI</b>	<b>ASILIMIA</b>
Kidato cha Pili	30	30	100%
Kidato cha Tatu	30	30	100%
Kidato cha Nne	30	30	100%
Walimu wa Kiswahili	6	6	100%

Utafiti huu ulikuwa na jumla ya wanafunzi 90, wanafunzi wa kidato cha pili walikuwa 30, kidato cha tatu wanafunzi 30 na kidato cha nne wanafunzi 30 na mwalimu mmoja mmoja anayefundisha somo la Kiswahili kutoka shule teule na hivyo kufanya jumla ya walimu 6. Wanafunzi wa kidato cha pili walikuwa 5 kutoka kila shule teule. Idadi hiyo ilivihusu pia vidato vya tatu na nne na hivyo kufanya jumla ya watafitiwa wote 90. Vidato hivi tulivitumia kwa kuwa mada hii inafundishwa kuanzia kidato cha pili na huwa inarudiwa tena kidato cha nne. Kidato cha tatu hakuna mada ya mofimu ila tulilazimika tupime kiwango cha uelewa kwenye utafiti wetu ili tuweze kupata picha ya kiwango cha maarifaa waliyonayo juu ya mada hiyo toka walipojifunza walipokuwa kidato cha pili mpaka muda huo. Pia mwalimu 1 anayefundisha Kiswahili alihusika kutoka kila shule teule. Kwa kuwatumia walimu wanaofundisha Kiswahili tuliweza kuelewa hali hii ya kiwango cha uelewa wa mofimu kwa wanafunzi wa sekondari kama inasababishwa na walimu wanaofundisha somo hilo. Mgawanyo huo wa wanafunzi ulizingatia jinsi ambapo kulikuwa na wavulana 45 na wasichana 45 kutoka kwenye madarasa ya utafiti.

### **3.6 Aina za Data Zilizokusanywa**

Kitchin na Rob (2014:6) wanaeleza data ni habari juu ya watu, nchi, uchumi, matukio au hali ya vitu mbalimbali. Mligo (2012) anasema kuna aina mbili za data ambazo ni data za msingi na data za upili. Katika utafiti huu tulihusisha aina zote mbili za data. Data za msingi ambazo tulizipata kutoka kwa watafitiwa teule na data za upili ambazo tulizipata kutoka maktabani.

#### **3.6.1 Data za Msingi**

Kothari (1992:95) anasema data za msingi ni data halisi kwa maana kwamba hukusanywa uwandani moja kwa moja tena kwa mara ya kwanza. Kimsingi utafiti wetu, ukusanyaji wa taarifa za awali ulikusudia kufanyikia katika shule sita za sekondari zilizoteuliwa ili kuchunguza ni kwa kiasi gani wanafunzi katika shule hizo wanafunzi hawafanyi vizuri katika mada ya mofimu tangulizi na mofimu fuatishi katika michakato ya uambishaji na unyumbuaji katika mizizi ya vitenzi vya maneno. Tulianza kukusanya data za msingi pindi tulipozitembelea shule za sekondari Idete, Upuge, Imalampaka, Puge, Manoleo na Uyui.

### **3.7 Mbinu za Kukusanya Data**

Katika utafiti huu tulitumia mbinu ya jaribio kama mbinu kuu na njia ya pili ilikuwa ya insha mbalimbali walizoandika wanafunzi kipindi cha utafiti ambamo kulikuwa na matumizi ya mofimu. Mbinu za dodoso na usaili pia zilitumika katika utafiti huu.

#### **3.7.1 Mbinu ya Jaribio**

Jaribio ni maswali yanayopima kama mada kuu iliyofundishwa imeelewka. Majaribio hutolewa katika muda maalum kama vile mwisho wa kufundisha mada

moja, mwisho wa juma, mwisho wa mwezi au mwisho wa muhula. Katika mbinu hii , mtafiti alilazimika kuandaa maswali mengi yaliyosaidia kupata taarifa za kutosha katika eneo hilo la mofimu. Mbinu hii ilituwezesha Kuona na kutathimini kwa kina kama malengo ya ufundishwaji wa mada ya mofimu kwa sekondari kama yamefikiwa na pia kujua kiwango cha uelewa wa wanafunzi katika mada ya mofimu.

Aidha tulitumia mbinu hii kupima vitu viwili kwa wanafunzi: mafanikio ya wanafunzi na kufanya kazi kwa vitendo kwa wanafunzi darasani na nje ya darasa, kwani hatuwezi kutenganisha upimaji wa mafanikio na upimaji wa utendaji.

Gunda (2014) anasema kuwa baada ya kufundisha somo au mada fulani upimaji kiasi gani wanafunzi wameelewa hufanyika. Kwa maneno mengine, tunapima wanafunzi wanaweza kufanya nini kutokana na wanavyofundishwa.

Tuliandaa majaribio mbali mbali waliyopewa wanafunzi ambayo yalipima ngazi ya chini na ngazi ya juu za upeo wa akili (kumbukumbu, ufahamu, uchambuzi, uunganisho na tathmini). Maswali hayo yalikuwa mchanganyiko. Tulichanganya aina zote za maswali fungo na yasiyo fungo ili kuepuka mapungufu ambayo yangeweza kujitokeza katika kutumia mbinu hizi mbili, ikizingatiwa kuwa kila moja ina mapungufu yake. Maswali fungo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua majawabu na ni rahisi kujibu na pia inasaidia kupata majibu mahususi na huokoa muda. Aina ya pili ya maswali ya jaribio ni yale yasiyo fungo (huru) ambayo hutoa fursa au uhuru kwa watafitiwa kueleza wanachokijua. Pia husaidia kupata taarifa nyingi zaidi.

Kimsingi aina hizo za maswali zikitumika kwa pamoja kila moja husaidia kuziba mapungufu ya nyenzake. Mbinu ya jaribio tulitumia kwa kuwa inafaa kukusanya data katika kundi kubwa la watu kwa muda mfupi sana. Maswali hayo tuliyatoa na kusahihisha papo kwa papo. Aidha ni njia rahisi na ya haraka katika kukusanya na kuzichambua data. Tulipokuwa tunatoa ripoti za maendeleo ya wanafunzi kwa kawaida tulitumia kazi mbali mbali walizokuwa wamepewa ambazo ni majaribio na uandishi wa insha.

### **3.7.2 Mapitio ya Insha**

Hapa tutajishughulisha na insha anuai zilizoandaliwa ambazo ziliwa na matumizi ya mofimu. Kuna aina kuu mbili za insha: Isha za Ubunifu na Insha za Kiuamilifu.

#### **3.7.3.1 Insha za Ubunifu**

Hizi ni insha ambazo mwanafunzi huhitaji kubuni maudhui, mazingira, wahusika nk. Kulingana na swali analorejelea. Tulitumia insha za mdokezo ambapo mwanafunzi alipewa kifungu cha maneno kinachopaswa kujitokeza katika insha yake. Baadhi ya insha za namna hii ziliwa zimetangulizwa na kisha kumtaka mwanafunzi akamilishe, na nyinginezo ziliwa na kimalizio. Japo mwanafunzi ana uhuru wa kuiendeleza insha yake atakavyo, ni sharti ajifunge katika maudhui yanayojitokeza katika mdokezo alipewa. Kwa hivyo, kabla ya mwanafunzi kuiendeleza insha yake ilikuwa ni sharti atambue maudhui yaliyokusudiwa na mtahini.

Tuliandaa insha zenye mjazo wa aina za mofimu, alomofu za utendea na mofimu za mnyambuliko ambazo mwanafunzi alizitumia katika kukamilisha insha yake. Mwanafunzi alipokuwa anajaza nafasi zilizoachwa wazi ili kukamilisha insha husika,

ilitusaidia kupima kiwango cha uelewa wa wanafunzi walionao juu ya mada ya mofimu.

### **3.7.3.2 Insha za Kiuamilifu**

Haya ni maandishi yenye mtindo maalum na hutumika katika mazingira halisi kwa kuzingatia mtindo huo rasmi. Ubunifu wa mwanafunzi hauwezi ukaathiri mtindo wa insha hizi. Kwa hiyo anachohitajika kuzingatia zaidi ni mtindo wa utunzi , mada na hija muhimu.

Katika kutumia mbinu hii tuliandaa insha mbalimbali, na kwa kupitia insha walizoandika wanafunzi walengwa kama sehemu ya majoribio au kazi za nyumbani, tulichunguza matumizi ya aina za mofimu, njeo, hali, ngeli, alomofu za utendea na mofimu za mnyambuliko.

### **3.7.4 Dodoso**

Kwa mjibu wa Kothari (1990), dodoso ni njia ya kukusanya data ambapo mtafiti huandika maswali na kisha kuyapeleka kwa watoa taarifa ili wayajibu na baadaye kumrudishia mtafiti yakiwa tayari yameshajibiwa. Wataalamu mbalimbali kama vile William (2011), Kothari (2008), Caesar (1998), MSSabila na Kinunda (2009) wanabainisha kuwa zipo aina mbili za maswali ya dodoso. Aina ya kwanza ya maswali ya dodoso ni maswali fungo ambayo hayampi uhuru mtafitiwa kutoa maoni yake mwenyewe bali mtafiti hutoa maswali na majibu kadhaa ili kumpa fursa mtafitiwa kuchagua jibu lililo sahihi zaidi.

Aina ya pili ya maswali ya dodoso ni maswali yanayohitaji maelezo kutoka kwa watafitiwa. Aina hii ya maswali humfanya mtafitiwa kuwa huru kueleza maoni na

hisia zake juu ya kile kinachoulizwa na mtafiti na husaidia kupata taarifa nyingi, kujua maoni ya watu kuhusu dhana anayoitafiti nk.

Kutokana na umuhimu wa kila aina ya maswali ya mbinu ya dodoso mtafiti alitumia aina zote mbili za maswali ya dodoso, ili kila aina moja ya maswali iweze kuziba pengo la aina nyingine ya maswali na kupunguza mapungufu ambayo huweza yakatokea pindi ambapo mtafiti angaliamua kutumia aina moja tu ya maswali ya dodoso. Mtafiti aliweza kutumia aina hii ya dodoso kwa kuandaa maswali yaliyokuwa na matumizi mbalimbali ya mofimu kwa ajili ya watafitiwa wanafunzi na maswali yaliyowataka walimu wanaofundisha somo la Kiswahili waweze kutoa maoni yao juu ya ufundishaji wa mada ya mofimu katika muhtasari wa Kiswahili wa mwaka 2010 unaotumika sasa.

Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata majibu ya swali namba *moja* ambalo lilihitaji kujua kiwango cha uelewa wa mofimu za uambishaji na unyambulishaji wa maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania pia kupata majibu ya swali namba mbili lililohitaji kujua sababu zinazosababisha uelewa wa mofimu uambishaji na unyambulishaji wa maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania utakaodhihirika kwenye swali namba moja.

### **3.7.5 Mbinu ya Usaili**

Mulokozi (1983) anaeleza kwamba mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana au simu, barua pepe kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainsishwa. Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu hii inamsaidia mtafiti kuweka bayana istilahi ambazo hazieleweki kwa watu walioulizwa. Mbinu hii pia humuwezesha mtafiti kupata taarifa za ziada na za kina.

Kothari anaendelea kueleza kuwa mbinu hii inamruhusu mtafiti kuuliza masuali ya ziada na kumuwezesha kuwa karibu na watoa taarifa. Walliman (2011) amegawa mbinu ya usaili katika aina tatu ambazo ni usailiwa ana kwa ana, usaili wa kikundi na usaili wa kutumia simu (mtandao). Hata hivyo, katika utafiti huu, mtafiti alitumia kwa kuwasaili watafitiwa wake wanafunzi walipokuwa wanajibu swali na 13 na 14 kuhusu lugha ya Kiingereza kuendelea kutumika kufundishia na kutumika katika mawasiliano ya kawaida katika shule za sekondari Tanzania na wanafunzi kutokua na utamaduni wa kujisomea wanapokuwa nyumbani, kwa kutumia maswali wazi yasiyofunge akayagawa kwa watafitiwa wake na akawafanya usaili wa ana kwa ana kwa lengo la kupata data za uhakika.

Aidha, mtafiti alitumia mbinu hii kwa sababu kadhaa, kwanza, ni kwa ajili ya kupata uthabiti wa majibu ya maswali ya majaribio yaliyohusu aina za mofimu na mnyambuliko wa vitenzi vyta maneno ya Kiwsahili sanifu. Pili, ni rahisi kwa mtafiti kudhibiti sampuli yake kwa wepesi na kwa usahihi zaidi. Tatu, mtafiti alitaka kupata data za utafiti huu ambazo ni majibu ya watafitiwa yaliyotokana na majaribio, maswali ya papo kwa papo na insha zilizoandikwa na wanafunzi ili kukidhi lengo la pili la utafiti. Hii imewezekana kwa sababu mtafiti alipata fursa ya kuwahojiwa ana kwa ana na kuwauliza maswali na kurikodi majibu yao papo kwa papo wakati mahojiano yao yanaendelea.

Pia maswali ambayo yalikosa majibu aliweza kuyatafutia ufumbuzi papo kwa papo. Nne, ilikuwa ni rahisi kwa mtafiti kukusanya taarifa nyingi na kwa kina zaidi kwa sababu watafitiwa waliweza kuuliza maswali na mtafiti alikuwa na uhuru wa kuuliza

maswali ya ziada fursa ambayo isingepatikana katika mbinu nyingine za kukusanya data kama vile hojaji na nyinginezo.

### **3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data**

Uchambuzi wa data kwa mjibu wa Kothari (2013), ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Hoja hii ilijadiliwa hapo awali na Biklen na Bagdan (1992) wakinukuliwa na Omari (2011) anaeleza kuwa hii ni hatua muhimu sana katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti husika. Data zilizokusanywa ambazo ni mofimu zinazopatikana kwenye maneno ya Kiswahili zilipangwa kulingana na malengo ya utafiti huu kiasi cha kuwezesha kuchunguzwa kwa urahisi. Katika utafiti huu data ziligawanywa kutegemea aina ya data kwa kigezo cha sifa ya data kuendana na malengo ya utafiti huu. Baadhi ya makundi hayo ni mofimu tangulizi, mofimu fuatishi, mofimu za njeo na mofimu za utendea. Kanuni zinazotawala katika mnyambuliko wa vitenzi pamoja na uandishi wa insha ziliwakilisha kundi la pili la data za utafiti.

### **3.9 Maadili ya Utafiti**

Mligo (2012) anasema maadili ni kanuni zilizowekwa na kukubaliwa na jamii ili zitumike kuongoza mwenendo wa maisha na tabia halisi ya maisha ya mwanajamii husika. Pond (1992) anafafanua maadili ya utafiti ni pamoja na haki ya kuwa na usiri, yaani mtafiti hatatoa siri ya mtafitiwa. Pia ameeleza kuwa haki ya mtafitiwa ni kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu pia haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Sisi kama watafiti tulizitambua haki hizi na kuzitekeleza kwa kuhakikisha mtafitiwa

anapata matokeo ya utafiti uliofanywa, kuwathamini na kutokuwabagua kulingana na tofauti ya madarasa yao. Mtafiti alihakikisha watafitiwa wanakuwa salama wakati wote wa utafiti na kwamba tatizo lolote lingejitokeza ingekuwa ni juu ya mtafiti mwenyewe.

### **3.10 Hitimisho**

Sura hii imewasilisha vipengele anuai ambavyo vinahusiana na mbinu ya utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa ni eneo la utafiti, wahusika lengwa ambao walikuwa ni wanafunzi 90 na walimu 6 walioteuliwa kutoka kwenye shule teule. Vilevile kipengele cha sampuli na usampulishaji vimejadiliwa kwa mapana yake. Kipengele hiki kimehusisha sampuli za shule sita. Aidha mbinu mbili zilizotumika wakati wa kukusanya data ambazo ni mbinu ya jaribio na mbinu ya mapitio ya nyaraka. Ukusanyaji na uchambuzi wa data kwa njia zake pia zimeelezwa kwa kina zaidi na mwisho maadili ya utafiti yameelezwa katika sura hii.

## **SURA YA NNE**

### **4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI**

#### **4.1 Utangulizi**

Sura hii inawasilisha, kuchambua na kujadili matokeo ya utafiti huu ambayo yalipatikana kutoka katika vyanzo anuwai ambavyo ni wanafunzi wa sekondari kidato cha pili, tatu na nne, pia walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule teule. Matokeo haya yamepatikana kutohata na utafiti wa uwandani na makitabani. Uwasilishaji na mjadala wa matokeo vimefanyika kwa kuzingatia lengo la jumla na malengo mahususi katika kufuata misingi na kanuni za kiunzi cha nadharia ya kiisimu ya utambuzi kilichoongoza utafiti huu.

#### **4.2 Taarifa ya watafitiwa**

Kimani (2015), anawanukuu Mugenda (2003), Kothari (2004) na Orodho (2003), wakisema kuwa taarifa za wahojiwa hutoa matokeo yanayoweza kutegemewa kwa kukipa kila kipengele uhalisia unaofaa. Matokeo haya yanaweza kulinganishwa na idadi nzima ya watu kwa kuwa sifa za sampuli iliyotumika ni kielelezo mwafaka cha idadi hiyo. Kigezo cha jinsia ya wahojiwa kilizingatiwa ili kuimarisha ubora wa data.

Taarifa hizi za wahojiwa ni kama ifuatavyo:

##### **4.2.1 Walimu wa Somo la Kiswahili**

Idadi ya walimu waliolengwa walikuwa ni 6 na ambao ni sawa na 100% walishiriki kati yao wanawake 4 (66.6%) na wanaume walikuwa 2 (33.3%). Kuhusu uzoefu kazini walimu 4(66.6) walikuwa na miaka kati ya 2 - 4, mwalimu 1(16.15%) alikuwa na miaka 5 na mwalimu 1alikuwa na miaka 22 kazini. Demografia hii inaonesha

wengi wa walimu waliohojiwa hawakuwa na muda mrefu kazini kwa kuwa ni idadi kubwa zaidi ikilinganishwa na walimu wazoefu. Uwiano wa walimu wa kiume na wale wa kike ulikuwa kama ifuatavyo: walimu wa kike walikuwa 4 sawa na 66.7% na walimu wa kiume walikuwa 2 sawa na 33.3%. Idadi hii inatokana na jumla ya shule zote 6 zilizo teuliwa kwenye utafiti.

#### **4.2.2 Idadi ya Wanafunzi**

Wanafunzi wa sekondari waliotafitiwa walikuwa 90, ingawa baada ya kukusanya hojaji mtafiti alibaini kuwa kulikuwa na hojaji 3 hazikujazwa kikamilifu, 1 kati ya hizo haikujazwa kabisa na 2 hazikujazwa maswali 2 ya mwisho kama jedwali na. 4.1 hapa chni linavyoonesha:

#### **Jedwali Na.4.1: Ujazaji wa hojaji Kiidadi na kwa Asilimia**

Hojaji	Haikujazwa kabisa	Zilijazwa kiasi	Zilijazwa kikamilifu	Idadi ya hojaji
Idadi ya hojaji	1	2	87	90
Asilimia	1.1%	2.2%	96.7%	100%

Hivyo waliojaza kikamilifu hojaji walikuwa 87 sawa na 96.7% ya sampuli iliyokusudiwa na wanafunzi 3 sawa na 3.3 hawakujaza hojaji vizuri. Wanafunzi hao waligawanyika katika vidato kama ifuatavyo; kidato cha pili wanafunzi 30 sawa na 100%, kidato cha tatu wanafnzi 30 sawa na 100% na kidato cha nne wanafunzi 30 sawa na 100%. Wanafunzi hawa wa kidato cha pili mpaka cha nne walihusika katika utafiti huu kwa kuwa mada hii inafundishwa katika vidato hivyo. Kuhusu jinsia ya wanafunzi hao walikuwa kama inavyoonekana kwenye jedwali na. 4.2 hapa chini ambapo wasichana walikuwa 45 sawa na 50% na wavulana 45 sawa na 50%.

Hojaji 90 zilitolewa na mtafiti sawa na asilimia 100, kati ya hizo 87 zilijazwa kikamilifu na watafifiwa sawa na 96.7%, hojaji 2 sawa na 2.2% hazikujazwa baadhi ya maswali yaliyowataka watafifiwa watoe mchango wao wa mawazo kuhusu lugha ya Kiingereza kuendelea kutumika kufundishia na kutumika katika mawasiliano ya kawaida na hojaji 1, sawa na 1.1% haikujibiwa kabisa.

#### **Jedwali Na. 4.2: Idadi ya wanafunzi watafifiwa sekondari kwa jinsi zao**

JINSI	IDADI	ASILIMIA
Wavulana	45	50%
Wasichana	45	50%
Jumla	90	100%

Jedwali hilo hapo juu linafafanua idadi kuwa kati ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu, 45 sawa na 50% ni wavulana na wasichana walikuwa 45 sawa na 50% na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi 90 sawa na 100%.

#### **4.3 Kiwango cha Uelewa wa Wanafunzi Kuhusu Mofimu**

Kipengee hiki ni katika kujabu lengo mahsus la kwanza la utafiti huu ambalo lilikuwa kupima uelewa wa mofimu tangulizi na mofimu fuatishi za unyumbuaji katika mizizi ya vitenzi vyta maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania. Utafiti huu ulikusudia kubaini kama wanafunzi wa sekondari wanaelewa kuhusu mada ya mofimu na aina zake, pia kanuni zinazotumika katika mnyambuliko wa maneno ya Kiswahili sanifu. Ili kufikia lengo hilo mtafiti aliandaa hojaji kwa ajili ya makundi makuu mawili ambayo yalikuwa ni wanafunzi 90 wa sekondari na walimu wao 6 ambapo mtafiti

alichukua mwalimu wa Kiswahili mmoja mmoja kwa kila shule. Pia mtafiti alianda majaribio ya aina mbili ambayo ni maswali ya isimu kuhusu mofimu na maswali ya insha aliyoyagawa kwa wanafunzi teule kuanzia kidato cha pili mpaka kidato cha nne na utungaji wa insha za ubunifu na insha za uamilifu kwa wanafunzi wa sekondari.

#### **4.4 Kiwango cha Uelewa wa Mofimu za Uambishaji na Unyambulishaji wa Maneno ya Kiswahili Sanifu**

Uambishaji ni mchakato mmoja wapo unaotumika katika kuunda maneno katika lugha. Nyangwine na Masebo (2007), Masamba (2004) na TUKI (1990) wanauona uambishaji kuwa ni uongezaji wa mofu (mofimu) kabla ya mzizi wa neno. Swali namba moja la utafiti lilihusu kutambua uelewa wa wanafunzi wa sekondari kuhusu mofimu za uambishaji, unyambulishaji na kanuni zinazotawala katika mnyambuliko wa maneno ya Kiswahili sanifu. Baada ya kutoa kazi mbalimbali kwa wanafunzi zikiwemo za ujazaji wa dodoso na uandishi wa insha zilizotokana na mada walizokwisha kujifunza, majibu ya wanafunzi yalionekana kama ifuatavyo;

**Jedwali Na.4.4: Uelewa wa Wanafunzi Kuhusu Mofimu Za Uambishaji**


KID ATO	ID AD I	AINA YA MASWA LI YALIYO TOLEW A	MAENE O WALIYO FANYA VIZURI	WANA FUNZI	% YA UELE WA	MAENE O YALIYO KUWA NA UTATA	WANA FUNZI	ASILI MIA
II	30	Kujazad odoso, kubainis ha mofimu awali na tamati na uandishi wa insha.	Maswali ya jaribio yaliyohus u aina, dhima ya mofimu na alomofu,m zizi na shina la kitemzi wanafunzi walifanya vizuri	21	68%	Swali na.2 lilihusu kutunga sentensi kwa kutumia vitenzi katika kauli mbalimba li kwenye maswali ya insha.	9	32%
III	30	Kujaza dodoso, kubainis ha mofimu awali na tamati na uandishi wa insha.	Maswali ya jaribio yaliyohus u aina,, dhima ya mofimu na alomofu,m zizi na shina la kitemzi wanafunzi kidato cha 3 ufaulu ulikuwa chini ya wastani.	14	54%	Katika kipengele cha uainishaji wa aina za mofimu na matumizi ya mofimu za njeo, hali, ngeli, aina za viambishi na mofimu za utendea katika hotuba na katika majadilia no katika swalii na.1	16	46%

						na 3		
IV	30	Kujaza dodoso, kubainis ha mofimu awali na tamati pia uandishi wa insha.	Katika kipengele cha ubainishaji wa mofimu awali na fuatishi kidato cha nne walifanya vizuri	17	51%	Katika kipengele cha uainishaji wa aina za mofimu na matumizi ya mofimu za njeo, hali, ngeli, aina za viambishi na mofimu za utendea katika hotuba na katika majadilia no katika swalii na.1 na 3	13	49%

Data katika jedwali hapo juu zinaonesha matokeo yaliyopatikana baada ya wanafunzi wa kidato cha pili, tatu na nne kujibu maswali ya dodoso yaliywataka kubainisha mofimu awali, tamati na uandishi wa insha zilizokuwa zinazelea matumizi ya mofimu. Matokeo ya naonesha wanafunzi 21 kati ya 30 wa kidato cha pili walipata 70% walipokuwa wanajibu swal namba 2 lililowataka kutunga sentensi kwa kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali na maswali ya jaribio yaliyohusu aina na dhima ya mofimu, alomofu, mzizi na shina la kitenzi. Ufaulu wao ulikuwa juu ya wastani na wanafunzi 9 ufaulu wao ulikuwa 30% chini ya wastani.

Wanafunzi wa kidato cha tatu walipokuwa wanajibu maswali ya jaribio yaliyohusu aina na dhima ya mofimu na alomofu, mzizi na shina la kitenzi, ufaulu wao ulikuwa chini ya wastani ambapo wanafunzi 14 kati ya 30 ufaulu wao ulikuwa 49% na wanafunzi 16 kati ya 30 ufaulu wao ulikuwa 51% katika kipengele cha uainishaji wa aina za mofimu na matumizi ya mofimu za njeo, hali, ngeli, aina za viambishi na mofimu za utendea katika hotuba na kwenye majadiliano katika swal na.1 na 3 na kidato cha nne matokeo yao hayakuwa mazuri walipokuwa wanashughulikia kipengele cha uainishaji wa aina za mofimu na matumizi ya mofimu za njeo, hali, ngeli, aina za viambishi na mofimu za utendea katika hotuba na kwenye majadiliano katika swal na.1 na 3. Matokeo yanaonesha wanafunzi 17 kati ya 30 ufaulu wao ulikuwa 51% ambapo wanafunzi 13 kati ya 30 ufaulu wao ulikuwa 49%.

Mfano wa majibu yasiyo sahihi ni kama inavyodhirishwa na kilelezo na. 4.1 hapa chini.



#### Kielelezo Na. 4.1: Mfano wa majibu yasiyo Sahihi ya Maana ya Mofimu (kidato cha 3)

Utafiti pia umebainisha kuwa wanafunzi wa kidato cha pili wamepata alama juu ya wastani kwa kuwa mada hiyo wamejifunza muda sio mrefu mpaka walipokutwa na mtafiti. Jambo la kuzingatia hapa ni kwamba wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne walionekana kuwa na umahiri mdogo kutokana na sababu kadhaa ambazo tutaziainisha tutakapokuwa tunajibu swalii la pili la utafiti huu.

##### 4.4.1 Uelewa kuhusu mofimu za mnyambuliko wa vitenzi

Katika sehemu hii tunaonesha kiwango cha uelewa wa watafitiwa katika maumbo ya mofimu zinazotumika katika unyambulishaji wa maneno ya Kiswahili. Kwa mujibu wa data mofimu zinazopachikwa katika unyambulishaji hujulikana kuwa ni uongezaji wa mofu au viambishi baada ya mzizi wa neno. Viambishi vya mnyambuliko vinavyotokea katika vitenzi vya maneno ya Kiswahili sanifu ni viambishi vya utendeshi {-esh-}, {-z-}, {ish}, utendana {-an-}, umbo la utendea {-e na -i}, umbo ia utendwa {-w-}, mofu ya utendana {-an-} na mofu ya kutendeka {ek} ambavyo huongezwa baada ya mzizi wa neno. Uelewa huu ulionekana kwa

wanafunzi wa kidato cha pili walipokuwa wanashughulikia swali namba moja ambalo likuwa ni jaribio lenye mchanganyiko wa maswali ya mofimu.

Uongezaji wa mofu hizi baada ya mzizi wa neno huzalisha kauli mbalimbali hasa kwenye vitenzi, kauli ambazo walikuwa wanazishughukia kwenye swali namba 2 lililohusu kutunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa:

Panga – tendea, tendwa, tendewa na tendeka

Taga – tendwa, tendeka, tendana na tendesha

Hama – tendea, tendana, tendeana na tendwa

Chukua – tendeka, tendesha, tendea na tendewa

Twa – tendea, tendewa, tendwa na tendesha.

Majibu halisia ya viambishi yangepaswa yawe jedwali na.4.4 linavyotanabaisha kuonesha namna viambishi vinavyopachikwa baada ya mzizi wa maneno ya Kiswahili.

#### **Jedwali Na.4.5: Viambishi vya unyambulishaji**

Neno	Mnyambuliko	Ubainisho wa mofu nyambulishi
Beba	Bebeshana	<i>beb-esh-an-a</i>
Pokea	Pokezana	<i>poke-z-an-a</i>
fagia	Fagiliwa	<i>fagi-li-wa</i>
Soma	Somesheana	<i>som-esh-e-an-a</i>
Piga	Pigiliwa	<i>Pig-il- iw-a</i>
Pendeza	Pendezeshwa	<i>Pendez-esh-w -a</i>
Kata	Katizana	<i>Kat-iz-an-a</i>

#### **4.4.2 Kauli zinazotokana na unyambulishaji wa vitenzi vyta maneno ya Kiswahili sanifu**

Ni vizuri kuelewa kwamba sio vitenzi vyote vinanyambulika katika kila kauli. Mtafiti aliangalia kauli ya kutenda, kauli ya kutendea, kauli ya kutendana, kauli ya kutendeana, kauli ya kutendwa, kauli ya kutendewa, kauli ya kutendeka na kauli ya kutendesha. Kauli hizi zilishughukiwa wakati wanafunzi walipokuwa wanajibu maswali ya jaribio na swali namba 2 lililokuwa linawataka wanafunzi watunge sentensi wakitumia vitenzi mbalimbali katika kauli walizopewa.

Mtafiti aliweza kuandaa na kuwapa watafitiwa maswali yanayohusu ubainishaji na utumiaji wa alomofu za utendea katika mizizi ya vitenzi vyta Kiswahili sanifu. Hali ilikuwa kama ifuatavyo:-


##### **Jedwali Na. 4.6: Uelewa wa mofimu za utendea katika mnyambuliko wa vitenzi**

KID AT O	IDADI YA WATA FITIW A	AINA YA MASWALI	IDADI YA WANAFU NZI WALIOFA NYA VIZURI	ASILIMIA YA UELEWA	IDADI YA WANAFUNZI WALIOFANY A VIBAYA
II	30	1.Kubainisha alomofu za utendea [ i na e ] 2.kutaja aina za mofimu katika lugha ya Kiswahili. 3..kuunda maneno mbalimbali ya Kiswahili kwa kutumia kauli/hali mbalimbali	18	52	12 (48%)
	30	1.kubainisha alomofu za	14	48%	16 (52%)

III		<p>utendea[<i>i na e</i>]</p> <p>2.kuunda maneno ya Kiswahili kwa kutumia kauli mbalimbali</p> <p>3.kubainisha mofu tangulizi katika mzizi wa kitenzi[a,na,li,ta me,ha,si]</p> <p>4.kubainisha mofu fuatishi katika mnyambuliko wa vitenzi.[esh, ish, an, ez, iz, ek, ew,iw]</p>			
IV	30	<p>1.Kubainisha alomofu za utendea [ <i>i na e</i> ]</p> <p>2.kuunda maneno ya Kiswahili kwa kutumia kauli mbalimbali</p> <p>3.kubainisha mofu tangulizi katika miziz wa kitenzi [a,na,li,ta,me ha,si ]</p> <p>4kubainisha mofu fuatishi katika mnyambuliko wa vitenzi [esh,ish,an,ez,iz,e k,ew,iw ]</p> <p>5.kufafanua kanuni zinazotawala mnyambuliko wa vitenzi</p>	13	41%	17(59%)

Jedwali na.4.5 hapo juu linaonesha hali halisi ya uelewa wa mofimu kwa wanafunzi wa sekondari ambapo wanafunzi 16 (52%) wa kidato cha tatu na wanafunzi 17(59%) wa kidato cha nne walishindwa kubainisha mofu zinazolezea kauli za utendea, kutendeana, kutendana, tendeshana na kutendwa.

Kielelezo Na.4.2 hapa chini kinadhihirisha mifano ya majibu yasiyo sahihi kuhusu uelewa huu.



**Kielelezo Na. 4.2: Mfano wa majibu yasiyo sahihi ya kazi za viambishi (Kidato cha Tatu).**

Hata hivyo, watafitiwa wa kidato cha pili wanafunzi 18 sawa na 52% waliweza kubainisha kauli ya kutenda, kutendewa na kauli ya kutendesha. Hata hivyo wanafunzi 12 sawa na 48% hawakuweza kuandika kauli za kutendana, kutendewa,

kutendwa ,kutendeka na kutendeana zilionekana hazieleweki kwa watafitiwa. Hali hiyo ilijitokeza pia kwa watafitiwa wa kidato cha tatu, wanafunzi 14 sawa na 52% walishindwa kuainisha kauli zote kama maswali yalivywataka wafanye. Kidato cha nne ni wanafunzi 13 sawa na 41% ndio waliweza kujibu maswali yote vizuri.

Matokeo ya utafiti wetu katika eneo hili la matumizi ya mofimu tunaweza kuyalinganisha na taarifa mbalimbali zinazotolewa na baraza la mitihani la Tanzania. Kwa mfano taarifa ya watahini kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu kidato cha nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2014. Sehemu A ya mtihani wa mwaka 2014 ilihusu sarufi, mofimu za utendea. Mfano: Swali la 2: “Dada ameandika barua kwa baba.” Sentensi hii iko katika kauli gani” Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua kauli za vitenzi. Watahiniwa 347,855 sawa na 43.92% walichagua jibu B “kutenda” ambalo lilikuwa ni jibu sahihi. Pia Swali la 7: “Juma amefika na hatacheza mpira.” Kitenzi “hatacheza” kipo katika hali gani? lililenga kupima uwezo wa watahiniwa wa kutambua hali za vitenzi. Watahiniwa 278,635 sawa na 35.18% walichagua chaguo A “Ukanushi” ambalo ndilo jibu sahihi.

Mtihani wa mwaka (NECTA, 2015) Sehemu B, swali namba 6 lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lilimtaka mtahiniwa kueleza dhima za mofimu *li* kama ilivyotumika katika sentensi tano alizopewa. Swali hili ni mionganoni mwa maswali yaliyojibowi vibaya na watahiniwa wengi kutokana na 93.1% ya watahiniwa wote waliojibu swali hili kushindwa kueleza dhima za mofimu *li* kama ilivyotumika katika sentensi walizopewa hivyo kupata alama 0 hadi 1. Wanafunzi 5.1% walipata alama  $1\frac{1}{2}$  hadi 2


ambazo ni alama za wastani. Aidha, 1.8% pekee ndio waliojibu vizuri zaidi na kupata alama  $2\frac{1}{2}$  hadi 5.

#### **4.4.3 Kanuni Zinazotumika katika Mnyambuliko wa Vitenzi vyta Kiswahili Sanifu**

Michakato na kanuni zinazotawala kwenye mnyambuliko wa vitenzi vyta Kiswahili sanifu imejadiliwa na wanataluma mbalimbali kama vile mawazo ya Polome (1967) kuwa unyambulishaji tendea una uwezo wa kuunda maneno mengi mapya katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu.

Mofimu nyambulishi ya utendea ina alomofu mbili ambazo ni: {-i-}, {-e-}. Utokeaji wa alomofu hizi unaweza kurasmishwa kikanuni kwa pamoja kama ifuatavyo: alomofu {-i-} hutokea katika mazingira ambapo mzizi wa kitende una irabu (-a-, -i-, na -u-). Alomofu {-e-} hutokea katika mazingira ambapo mzizi wa kitende una irabu (-e-) na {-a-}.

Unyambulishaji tendea unaonesha kuwa una uwezo mkubwa wa kuunda maneno mbalimbali yenye sifa tofauti katika lugha. Kwa mujibu wa maswali yaliyotolewa kwa watafitiwa yakiwemo yale yaliyowataka waandike kanuni zinazotawala mnyambuliko wa vitenzi, kanuni hizo zilionekana hazijulikani vizuri kwa wanafunzi wa kidato cha nne ambapo ni wanafunzi 12 sawa na 36% kati ya 30 ndio walioweza kuziandika kanuni hizo wakati wanafunzi 18 sawa na 64% ya wanafunzi wakashindwa kuziandika kanuni hizo. Watafitiwa wa kidato cha pili nao walionekana kuwa na uelewa wa aina za mofimu kwa 68% na kushindwa kubainisha mofu za utendea ambapo ni 35.7% ndio waliweza kujibu maswali vizuri ya mofu za utendea kama kielelezo na. 4.3 hapa chini kinavyoonesha majibu ya mwanafunzi mmojawapo.



**Kielelezo Na. 4.3: Mfano wa majibu yasiyo Sahihi ya Wanafunzi Mmojawapo (Kidato cha Pili).**

Mtafiti amebainisha kuwa wanafunzi wa kidato cha nne walishindwa kubainisha alomofu za utenda { i na e } walipokuwa wanajibu swalii namba moja kwenye maswali ya insha lililokuwa linasema Bainisha matumizi ya mofimu za njeo, hali, ngeli, aina za viambishi na mofimu za utendea katika hotuba . Wanafunzi 13 kati ya 30 sawa na 41% ndio waliojibu swalii hilo kwa kuzitaja alomofu {i na e } vizuri na

wanafunzi 17 sawa na 59% hawakuweza kujibu swali hilo, watahiniwa 9 hawakujaza waliacha wazi na watahiniwa 8 walitaja mofimu zingine. Jedwali namba 4.3 hapo juu linaonesha kuwa wanafunzi wanapokuwa kidato cha pili wanaonekana kuwa na ufaulu wa juu ya wastani lakini kadiri wanavyoendelea na kidato cha tatu na nne uelewa wao huwa unaenda unashuka kama jedwali linavyojieleza.

#### **4.5 Sababu Zinazofanya Wanafunzi kuwa na Uelewa Mdogo**

Lengo la pili mahususi la utafiti huu lililenga kutafuta sababu za ufaulu ambaou ungedhihirika katika matokeo ya upimaji wa uelewa kadiri ya lengo mahususi la kwanza. Mtafiti alitafuta majibu ya lengo hili toka kwa watafitiwa wanafunzi na waalimu wao kwa njia ya dodoso. Matokeo yalionesha kuwa kuna sababu anuwai zinazofanya wanafunzi kuwa na uelewa mdogo wa mofimu hasa wanapokuwa kidato cha nne wanafunzi huonekana kana kwamba hawajajifunza mada hiyo. Baadhi ya sababu walisema husababishwa na:

- i. Mbinu ya kufundishia inayotumiwa na walimu wa sekondari kufundishia Kiswahili;
- ii. Lugha ya Kiingereza kuendelea kutumika kufundishia na katika mawasiliano ya kawaida katika shule za sekondari
- iii. Wanafunzi kutokuwa na muda wa kujisomea wanapokuwa nyumbani baada ya muda wa masomo na zile siku za mapumziko.
- iv. Matatizo yaliyomo kwenye mtaala wa sekondari
- v. Mapungufu ya mpangilio wa mada kwenye muhtasari wa Kiswahili sekondari

Pamoja na hizi sababu toka kwa watafitiwa, uchunguzi wa kina uliofanywa na mtafiti ulionesha kuwa wanafunzi hawako makini katika kufanya kazi zao za kitaaluma za darasani. Kwa mfano, kidato cha nne walitakiwa waandike insha ya athari za mitandao ya kijamii wao walijikuta wanaelezea faida tu bila kuangalia mitandao hii ina hasara gani kwa jamii. Umoja wa wakuu wa shule za sekondari nchini katika mikoa ya Katavi na Rukwa (TAHOSA) katika kikao chake cha mwaka 2012 baada ya matokeo ya mtihani wa kidato cha pili na cha nne walisema “madhara ya sayansi na teknolojia kwa wanafunzi ni makubwa na yanapelekea ufaulu duni kwa wanafunzi ambapo wanafunzi wamekuwa wakitumia muda mwingi kutizama runinga, internet na matumizi ya simu za mkononi”. Aidha walisema kuwa msukumo wa ndani wa kujifunza kwa wanafunzi siku hizi ni mdogo sana kwa hali hiyo wanafunzi wengi hawajitumi kujifunza na kujipatia maarifa wanapokuwa shulen na hata nyumbani ndio maana wanakosa maarifa ya kutosha ya kuwawezesha kufanya vema katika mitihani yao.

Hata hivyo mtafiti alipokuwa anafanya usaili na kukagua madodoso aliyokuwa ameyagawa kwa wanafunzi utafiti ulionesha mtafiti alibaini kuwa wanafunzi hawapati motisha ambayo itawafanya walifurahie somo na kulipenda.kuwa, hali hii si kwa somo la Kiswahili pekee ni katika masomo yote wanayojifunza shulen. Hali hii ilibainika walipokuwa anawasaili wanafunzi.

#### **4.5.1 Mbinu ya Kufundishia Inayotumiwa na Walimu wa Sekondari**

Jedwali lifuatato linaonesha matokeo ya majibu ya swali namba 3 ya dodoso la walimu ambalo lilijikita kwenye matumizi ya mbinu za kufundishia zilivyoweza

kutumiwa na walimu wa Kiswahili kufundishia mada ya mofimu. Jedwali Na 4.6 hapo chini linaonesha kuwa kati ya njia shirikishi na njia ya mhadhara zinazotumika kufundishia mada ya mofimu na mada zingine kwa ujumla ni njia ya mhadhara ndio njia inayo pendelewa zaidi sana na walimu wa sekondari.

**Jedwali Na.4.8: Mbinu za kufundishia na kujifunzia Wanazotumia Walimu**

<b>Idadi Ya Walimu</b>	<b>Kidato</b>	<b>Njia Iliyotumika</b>	<b>Asilimia</b>
4	II-IV	Njia ya mhadhara	66.7%
2	II-IV	Njia shirikishi	33.3%

Mtafiti alipofanya uchunguzi makini kwa kutumia mbinu ya usaili wa walimu na ushuhudiaji madarasani aligundua kuwa njia ya mhadhara ambayo walimu wa sekondari wanaitumia kufundishia sio rafiki kwa wanafunzi kujifunza kwa kuwa njia hii haimpi mwanafunzi nafasi ya kutoa alichonacho badala yake mwalimu ndie huonekana anajua kila kitu. Hali hii humfanya mwanafunzi asijifunze kwa ufanisi. Hali hiyo inaonekana kuitia data zilizopatikana kutokana na mbinu ya usaili tuliofanya ambapo walimu 4 kati ya 6 walioonwa na mtafiti, sawa na 66.7% walikuwa wanatumia njia ya mhadhara na njia ya maswali na majibu. Walimu 2 tu sawa na 33.3% kati ya 6 ndio walionekana wanafanya kazi pamoja na wanafunzi kwa kutumia njia shirikishi. Hali hii inaashiria kwamba walimu hawashughulikii mahitaji mahususi ya mwanafunzi mmoja mmoja katika mchakato wa ujifunzaji. Hii inaashiria pia kwamba mchakato wa ufundishaji bado kwa kiwango kikubwa unaegemea kwa mwalimu ingawa mtaala unasisitiza katika kutumia njia inayotumika.

#### **4.5.2 Lughya ya Kiingereza Kuendelea Kutumika Kufundishia na Kutumika katika Mawasiliano ya Kawaida**

Mtafiti alipokuwa anapitia majibu ya swali namba 14 lilouliza, Je, kuendelea kutumika kwa lugha ya Kiingereza kwa shule za sekondari kama lugha ya kufundishia na mawasiliano ya kawaida kunachangia kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mofimu? Likienda sanjari na swali namba 4 la usaili, matokeo ya utafiti yalifanana na uchanganuzi wa hoja uliofanywa na wataalamu mbali mbali yameendelea kudhihirisha matatizo ya kuendelea kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia, hasa elimu ya sekondari. Miongoni mwa wataalamu hao ni Mlama na Matteru (1978), Mkude (1982), Ciper na Dodd (1984), Roy-Campbell na Qorro (1996), Yahya-Othman na Batibo (1996). Katika utafiti, makala na machapisho yao mengine, wataalamu hao, na wengine wengi wamehoji na kudhihirisha kuwa, (i) Hivi sasa Kiingereza hakitumiki tena ipasavyo kama lugha ya kufundishia; na hivyo (ii) kuendelea kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia elimu ya upili kunakwamisha uwasilishi na upokeaji wa maarifa yaliyokusudiwa wanafunzi wayapate; (iii) kuendelea kutumia Kiingereza kunadumaza miongoni mwa wanafunzi weledi wa lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili kadharika, kama lugha za mawasiliano ya kitaaluma; (iv) kuendelea kutumia Kiingereza katika hali kama hiyo kunaondoa uwezekano wa kuendelea kufundisha vizuri Kiingereza.

Utafiti unaonesha kuwa wanafunzi wanakosa maarifa ya kutosha juu ya stadi mbali mbali za Kiswahili kwa kuwa lugha ya Kiswahili inatumika wakati wa kipindi cha Kiswahili tu. Matumizi ya lugha sahihi/inayofaa ya kufundishia kwa walimu na lugha ya kujifunzia kwa wanafunzi vilipimwa kama kigezo muhimu katika ufanisi

wa ufundishaji. Matokeo yanaonesha kwamba, kati ya vidato vitatu vilivyofanyiwa utafiti, ni 33.3% sawa na wanafunzi 30 waliweza kuandika insha zenyе mtiririko mzuri wa mawazo na 66.7% sawa na wanafunzi 60 hawakuweza kuandika insha vizuri. Hali hii inasababishwa na lugha ya Kiingereza kuendelea kutumika kufundishia na kutumika kama lugha ya mawasiliano kwani mwanafunzi awapo shuleni hulazimishwa kuongea Kiingereza muda wote ndani na nje ya darasa isipokuwa wakati wa kipindi cha somo la Kiswahili tu. Hali hii inaminya mwanya wa wanafunzi kuwa na umahiri wa mada ya sarufi kwa ujumla kwa sarufi ni elimu ya kupanga maneno kwa ufasaha. Maeleo hayo yanaweza kutafsiriwa kwa namna mbili tofauti. Kwanza, yanaweza kutafsiriwa kwa maana ya ufunzaji wa vipengele kama msamiati, utungaji wa sentensi, viashiria, vitenzi na kadhalika. Hapa kuna mambo kama methali, hadithi, vitendawili, itikadi na kadhalika.

Tafsiri ya pili ya maeleo haya huchukua yote yafunzwayo katika lugha fulani. Kama maeleo ya awali, sarufi ina vipengele tofauti tofauti. Ikiwa pamoja na kufunza maneno magumu, vitenzi, nyakati, matamshi, ngeli, vivumishi, majina, vielezi na viingizi. Tena, sarufi ni tawi la isimu. Mtafiti alipokuwa anashughulikia swali namba 4 katika kipengele cha usaili, aliwaliza wanafunzi kama lugha ya kiingereza kuendelea kutumika kufundishia na katika mawasiliano ya kawaida kwa shule za sekondari kunachangia kukosa maarifa ya kutosha katika mada ya mofimu. Matokeo ni kama yanavyoanishwa na jedwali na. 4.10 hapa chini.

**Jedwali Na.4.10: Lugha ya Kiingereza Kuendelea Kutumika kunaathiri Ujifunzaji wa Mofimu?**

NA.	SWALI LA DODOSO KWA WANAFUNZI.	NDIYO	HAPANA	SIJUI	JUMLA
1.	Kuendelea kutumika lugha ya Kiingereza kufundishia sekondari inaathiri ujifunzaji wa somo la Kiswahili.	80 (88.8%)	11 (11.2%)	0	90 (100%)
2.	Muda wa kujsomea nyumbani	33 (44%)	42 (56%)	0	75 (100%)

Majibu ya majadiliano ya wanafunzi na mtafiti juu ya swali hili yalionesha kuwa wanafunzi 80 sawa na 88.8% kati ya wanafunzi wote 90 walikubali kuwa hiyo ni sababu mojawapo kubwa ya kukosa maarifa ya mada ya mofimu katika shule za sekondari Tanzania. Idadi ndogo sana (wanafunzi 10, sawa na 11.2%) ndiyo hawakuonesha mwelekeo wowote kuhusu swali hili. Mtafiti alikubaliana na hoja hizo kwani kuna ushahidi mwangi ikiwa ni pamoja na uchache wa vipindi vyta somo la Kiswahili kwenye ratiba ikilinganishwa na masomo mengine na wanafunzi kulazimishwa kutumia lugha ya Kiingereza katika mawasiliano ya kawaida ndani na nje ya darasa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alisema “ Ni kazi ngumu sana kwa mwanafunzi wa sekondari kuwa na maarifa ya kutosha kwenye somo la Kiswahili kwa kuwa Kiswahili kinatumika kama lugha ya ziada maana mwanafunzi muda wote awapo shulenii analazimika kutumia lugha ya kiingereza na kuna badhi ya shule

mwanafunzi akionekana anaongea lugha ya Kiswahili huadhibiwa hivyo hali hii inachangia sana mwanafunzi kuwa na msamati mchache wa Kiswahili”.

Mwalimu mmoja alipoulizwa alisema, vipindi nya Kiswahili vilivyopangwa kwenye ratiba ya masomo ni vichache ikilinganishwa na somo la Kiingereza, kwa mfano: vipindi vitatu nya kiswahili kwa wiki (kwa ajili ya kidato cha I-IV) vilivyopangwa havitoshi kufundisha vipengele vyote nya sarufi na fasihi ya Kiswahili. Walimu wengi huwa hawamalizi kufundisha mada zote zilizoainishwa kwenye muhtasari kutokana na uchache wa vipindi.

#### **4.5.3 Wanafunzi kutokuwa na muda wa kujisomea**

Mtafiti vilevile alitumia hojaji kuwa uliza wanafunzi kama wanapata muda wa kutosha kujisomea wanapokuwa nyumbani. Majibu kutokana na majibu ya swali dodoso hili ni kama yanayoonekana katika jedwali na 4.11 hapa chini.

#### **Jedwali Na.4.11: Wanafunzi kutokuwa na Muda wa Kujisomea wanapokuwa nyumbani**

Na	Swali la dodoso la wanafunzi	Idadi ya shule za kutwa za kijijini	NDIYO	HAPAN A	Jumla ya wanafunzi
1.	Je, huwa unapata muda wa kujisomea unapokuwa nyumbani baada ya kutoka shuleni?	5	33 (44%)	42 (56%)	75
2.		1	12 (80%)	3 (20%)	15

Majibu ya swali dodoso hili kadiri ya jedwali na 4.11yalionesha kwamba wanafunzi 42 sawa na 56% kati ya wanafunzi 75 wa shule za kata za vijijini walionesha kuwa

hawapati muda wa kujisomea wawapo nyumbani kutokana na umbali mkubwa kati ya shule na nyumbani. Hivyo wanafunzi hufika nyumbani wamechoka hali hiyo huwafanya wasipate muda wa kujisomea .Wanafunzi 33 sawa na 44% kati ya wanafunzi 75 wa shule za kutwa za kata walikanusha kuwa hiyo sio sababu ya kuwafanya wawe na uelewa mdogo kuhusu mofimu kwa kuwa wao wamepanga jirani na shule hivyo hupata muda wa kutosha wa kijisomea kwani ifikapo saa 2:00 usiku huenda shulenii kujisomea mpaka saa 4:00 usiku.

Kwa upande wa shule ya mjini majibu yalikuwa tofauti na shule za kijijini ambapo mbinu ya usaili ilitumika. Wanafunzi 12 amba ni sawa na 80% walisema wanapata muda wa kutosha wa kujisomea wanapokuwa nyumbani.Walisema huwa wanapata masomo ya ziada yanayotolewa na walimu nje ya muda wa shule. Wanafunzi 3 sawa na 20% walisema hawapati hayo masomo ya ziada kwa kuwa wazazi/walezi wao hawana uwezo wa kuwalipia gharama hizo za masomo. Hivyo majibu ya utafiti yalioneshaa kuwa wanafunzi wengi wa shule za kutwa za kijijini hawapati muda wa kujisomea wanapokuwa nyumbani ukulinganisha na wanafunzi waishio mjini wao wanapata muda wa kujisomea kupitia hayo masomo ya ziada yanayotolewa nje ya muda wa shule.Utafiti huu wa kupata muda na kutopata muda wa ziada baina ya shule za kata za kijijini na za mjini ulibainika mtafiti alipokuwa anapima ufahamu wa mofimu kwa shule teule za sekondari.

#### **4.5.4 Upungufu kwenye Mtaala wa Somo la Kiswahili**

Mtaala wa elimu, kwa majibu wa Homby (2006), ni masomo yanayojumuisha mafunzo ya kozi fulani au jumla ya masomo yanayofundishwa shulenii, chuoni na kadhalika. Tylor (1949) anauona mtaala kuwa ni yale mambo yote yaliyoandalialiwa

kwa ajili ya kujifunza, yanayosimamiwa na shule ili kukamilisha malengo ya shule.

Sigalla (2003:4) akihitimisha fasili za wataalamu mbalimbali waliofasili mtaala anasema mtaala una mambo yafuatayo:-

Masomo ambayo ni msingi wa maarifa ya elimu.

Maarifa ambayo mwanafunzi anapaswa kuyapata.

Maarifa tarajiwa ndani na nje ya shule.

Nyaraka ambayo inajumuisha taratibu za kitaaluma.

Kwa kuzingatia mambo anuai yaliyomo kwenye mtaala na ambayo mwanafunzi anatakiwa ayapate kwa muda wote atakapokuwa shulenii, mtafiti kwa kutumia madodoso ya maswali ya walimu na mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na watafitiwa (walimu) aligundua kuwa mtaala wa elimu una mapungufu kadhaa yanayochangia mwanafunzi akose umahiri katika mada tunayoiangalia ya mofimu, ikizingatiwa kwamba elimu bora ni ile itakayowawezesha wanafunzi kufikia vigezo viwili: mosi, kuwawezesha wanafunzi kuwa na uwezo kitaaluma ambao huendana na kufikiri kwa mantiki, kutambua tatizo na kulitafutia ufumbuzi wake na kushiriki katika mijadala ya kitaaluma. Pili, kuwaandaa wanafunzi kuwa na uwezo wa kupambana katika ulimwengu wa kazi; elimu ambayo itampatia mwanafunzi stadi za kitaalamu kama vile stadi za mawasiliano na kazi husika.

Wakati tukitambua na kupongeza ongezeko katika usajili wa wanafunzi katika shule za sekondari miaka ya hivi karibuni, ni wazi kwamba ongezeko hili haliendi sambamba na nyenzo za kufundishia na kujifunzia zilizoko shulenii kwa kuwa mtaala na ujifunzaji ni vitu vinavyoenda pamoja na hii ikimaanisha kwamba mtaala mbovu unaweza kuathiri ubora wa taaluma inayokusudiwa. Tunavyoweza kuviona ni vitu

vinavyotokana na mtaala pamoja na athari za mtaala, na si mtaala wenyewe. Pia kipengele kingine kinachoonesha mapungufu ya mtaala ni kuhusu ufanisi wa mtaala wa elimu Tanzania. Mtaala uliopo haujitoshelezi katika kutoa wahitimu wenyewe uwezo wa kujitegemea.

Kipengele kingine kinachoonesha mapungufu ya mtaala ni kuhusu ufanisi wa mtaala wa elimu Tanzania. Mtaala uliopo haujitoshelezi katika kutoa wahitimu wenyewe uwezo wa kujitegemea. Walibainisha kwamba elimu iliyokuwa ikitolewa katika miaka ya 1980 na 1990 ilikuwa ikimwezesha mhitimu kuwa na mawazo ya kujitegemea katika ngazi yoyote ya elimu aliyofikia, na walibainisha pia kwamba kwani elimu inayotolewa siku hizi inamfanya mhitimu ategemee zaidi ‘kuajiriwa na kufanya kazi za ofisini’. Hii inatokana na mtaala wenyewe wa sasa ambao unatilia mkazo zaidi katika taaluma badala ya kutilia mkazo katika stadi za maisha (HakiElimu, 2010).

Hata hivyo kuna mabadiliko mengi ya mtaala ambayo yamefanywa katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Hali hii ilisababisha mkanganyiko kwa wadau. Wadau wengi walikosoa mabadiliko ya mtaala ambayo yamefanywa kwa haraka. Walimu waliukosoa serikali kwa kuanzisha mtaala ambao hauendani na mahitaji ya watu. Pia waliukosoa mwenendo wa serikali katika miaka ya hivi karibuni ambapo imekuwa ikifanya mabadiliko ya mtaala bila ya kuwahusisha wadau ukijumuisha walimu na wanafunzi. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja ambaye ni mwalimu alikuwa na haya ya kusema kuhusu mabadiliko ya mtaala: *Serikai imekuwa ikifanya mabadiliko ya mtaala kiasi cha kutuchanganya walimu. Kabla ya walimu hatujauzoea mtaala mpya, mabadiliko yanafanyika.*

Mwalimu mwingine anayefundisha somo la Kiswahili katika shule zilizoshiriki katika utafiti alilaumu mabadiliko ya mara kwa mara yanayofanywa katika mtaala, ambapo alisema “*hakuna mtaala maalum kwani mabadiliko ya mara kwa mara yamekuwa yakifanywa kwenye mtaala na hali hii hutuchanganya walimu.* Mwalimu mwingine alikuwa na haya ya kusema: *Mabadiliko ya mtaala yanapofanyika, hatupewi muda wa kutosha kuyaelewa kabla ya utekelezaji kuanza. Mara nyingi mabadiliko haya yanafanywa bila ya kuwahusisha wadau. Vilevile vitabu na vifaa vingine muhimu* *vya kufundishia na kujifunzia huwa havifiki kwa wakati pindi mabadiliko yanapofanyika.* *Kwa mfano tangu mabadiliko katika mtaala wa elimu ya msingi yatokee kuanzia darasa la kwanza mpaka la nne miaka mitatu iliyopita vitabu vya kiada vimeletwa vichache kwa baadhi ya masomo na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia. Je, unategemea walimu wafundishe vipi? Mtaala ni mpya ila vitabu ni vya zamani kwa baadhi ya masomo na vitabu vipyta kwa masomo mengine, hali hii inawezekana vipi?*

Swali hili pia lilijibiwa na mwalimu mmoja kati ya sita ambaye ni sawa na 16.7% aliyesema mtaala unafaa na unakidhi matarajio ya wanafunzi na walimu watano kati ya sita sawa na 83.3% walisema mtaala una mapungufu kwa kuwa mtaala tulionao hautoi fursa kwa mwalimu awe mbunifu, mtaala unamtaka ajikite kwenye maudhui ya mada husika yaliyopangwa na wizara ya elimu, hivyo mwalimu analazimika kuwa mtumwa wa mtaala na silabasi ya Kiswahili. Pamoja na hayo walimu waliojibu swali hili walitaja mapungufu mengine yafuatayo; -

Mtaala hautilii mkazo mada za isimu katika ngazi ya sekondari ndio maana hakuna vitabu vya kiada vya isimu ili hali sekondari kuna vitabu vya kiada vya fasihi kunzia kidato cha tatu hadi cha nne.

Hakuna maabara ya masomo ya lugha

Hakuna walimu wenyewe ujuzi wa isimu, walimu waliopo wanategemea vitabu vyatia ambavyo hutofautiana na hivyo kuwachanganya walimu na wanafunzi. Mada hazina mpangilio unaoelewaka kwani mada nyingi hujirudia katika vidato vyatia juu Baadhi ya vitabu vyatia kiada huhitilafiana kimaudhui hivyo huleta mkanganyiko Mipaka ya mofimmo kwa baadhi ya maneno ya Kiswahili si bayana

Hakuna semina za mada za isimu

Maelezo hayo ya walimu yanajibu swali lililolenga kujua mapungufu yaliyomo kwenye mtaala wa Kiswahili sekondari. Mapungufu namba (i) mpaaka namba (viii) ni sehemu ya mapungufu ya mtaala yanayo athiri kwa namna moja au nyingine ujifunzaji wa mada ya mofimmo sekondari hivyo kuwafanya wanafunzi kuwa na uelewa mdogo wa mofimmo tangulizi na fuatishi katika mizizi ya vitenzi vyatia maneno ya Kiswahili. Mapungufu kama hayo yalibainishwa pia na Mtana (1998), Msanjila (2005), Ndosi (2011) na Mbalamwezi (2012).

#### **4.5.5 Mapungufu ya Muhitasari wa Kiswahili Sekondari**

Mhitasari ni mwongozo unaotaja kwa kifupi tu mambo yote yanayotakiwa yafundishwe katika mwaka mzima, katika darasa furani au kwa miaka kadhaa kwa kila darasa kwa mpangilio maalumu. Muhtasari unaonyesha kitu gani kifundishwe kwenye somo, lini, kwa nani na kwa mbinu zipi. Swali lililohusu utoshelevu wa muhtasari wa Kiswahili wa mwaka 2005 liliulizwa kwa walimu wa Kiswahili. Hali ya mapungufu yaliyomo kwenye silabasi ilibainishwa na majibu yaliyotolewa na walimu, walisema kuwa mtiririko wa mada ulivyopangwa haukuzingatia kiwango cha uelewa na umri wa mwanafunzi. Mwalimu mmoja alisema kuwa mada

zilivyopangwa kwenye muhtasari haziendi sanjari na utaratibu wa uwasilishaji wa maarifa mapya kwa mwanafunzi, utaratibu unamtaka mwalimu anapofundisha aanze kufundisha vitu rahisi kwenda vigumu. Hali hii haijazingatiwa katika upangaji wa mada kwenye silabasi. Alisema kwa mfano mada ya ngeli za maneno ilitakiwa ifundishwe kidato cha pili na mada ya mofimu ifundishwe kidato cha tatu ili kuwe na mtiririko faafu wa kuhawirisha maarifa kwa mwanafunzi anapokuwa kwenye tendo la kujifunza.

Msanjila (2015) anafafanua mapungufu kadhaa ya muhitasari wa Kiswahili kwa kusema kuwa mada zilizopangwa kufundishwa kwa kidato cha I-IV kwa mjibu wa mhtasari wa 1996 ni hizi zifuatazo: Lugha, Fasihi Andishi na Fasihi Simulizi, Sarufi, Ufahamu , Utungaji, Utumizi wa Lugha na Historia ya Kiswahili. Kila mada ina vipengele vyake vidogovidogo vinavyopaswa kufundishwa katika kila kidato. Hii ina maana kwamba kila kidato hufundishwa mada hizi saba kwa viwango tofauti kulingana na kidato anachosoma mwanafunzi. Msanjila (kashatajwa), akimunukuu Kihore (2001), anabainisha kasoro mbalimbali zilizomo kwenye muhtasari. kama vile mada zilizopangwa kufundishwa hazitofautishi bayana viwango vya kidato. Pia mada hazizingatii maendeleo ya taaluma na mitazamo mipya ya kinadharia. Vipengele vidogo vinajirudia rudia katika kila mada bila ya kuonesha tofauti ya uchanganuzi wa kina wa mada kwa kila kidato. Ni rahisi kwa mwalimu asiye na uzoefu wa kutosha wa kufundisha somo la Kiswahili kurudia kufundisha mambo yaleyale katika vidato vinavyokaribiana kama vile kidato cha 1 na 2, kidato cha 3 na 4. Mwalimu mmoja katika mjadala alisema, *inashangaza kuona kwamba Kiingereza kinapewa vipindi 6 kwa wiki ikiwa ni mara mbili ya vile vya Kiswahili. Hata kama*

*kigezo kilichotumika kina lengo zuri la kuwapa wanafunzi muda mwangi wa kujifunza lugha ya kigeni wawapo shulen, bado kigezo hicho hakiwezi kuwa sababu ya msingi ya kukipunguzia Kiswahili idadi ya vipindi vyake kutoka vipindi 4 vya zamani hadi vipindi 3 vya sasa.*

Msanjila (2015) anaongeza kuwa zamani vipindi vya Kiswahili vilipokuwa 4 kwa wiki hakukuwa na mada nyingi za Kiswahili za kufundisha kuliko ilivyo sasa. Hatuoni kwa nini vipindi vipungue wakati mada za kufundisha zimeongezeka. Maana tunayoipata hapa ya kupunguza vipindi vya Kiswahili ni kwamba hii nayo ni sababu moja wapo inayowafanya wanafunzi wawe na uelewa mdogo wa mofimu kwa kuwa wanafunzi hawapati muda wa kufanya mazoezi ya kutosha kuhusu kanuni zinazotawala mnyambuliko wa mofimu katika mizizi ya vitenzi vya maneno ya Kiswahili, katika uandishi wa insha mbalimbali zinazobeba mofimu tangulizi na fuatishi.

#### **4.5.6 Maoni kuhusu Kiwango cha Uelewa wa Mofimu wa Wanafunzi**

Mtazamo wa walimu kuhusu kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu mofimu kilibainishwa na pia mtazamo hasi ambao jamii inao kuhusu somo la Kiswahili. Walimu waliohojiwa walisema haya kuhusu mtazamo hasi ambao jamii inao kuhusu somo la Kiswahili;

Serikali inathamini masomo mengine zaidi kuliko kiswahili. Mfano vyuo vikuu wanaopewa mkopo 100% ni wale wanaosoma sayansi.

Somo la Kiswahili linachukuliwa kuwa ni somo rahisi na ni mtu yejote anaweza kulisoma.

Somo la Kiswahili hudhaniwa kuwa ni somo la wanawake, wakati si kweli somo hili lina uzito sawa na masomo mengine.

Kuhusu uwiano uliopo kati ya mada za mofimu na mada nyingine za isimu, upitiaji wa muhtasari ulionesha hali halisi kama ilivyo kwenye jedwali na. 4.12 hapa chini.

#### **Jedwali Na: 4.12: Uwiano wa Mada ya Mofimu na Mada Zingine za Isimu**

Mada Za Isimu	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia	Maoni
Mada ya Mofimu (Sarufi)	68	75.5%	mada ni ngumu
Mada ya mofimu (Sarufi)	22	24.5%	mada ya mofimu sio ngumu
Mada zingine za isimu (Lugha, Fasihi Andishi na Fasihi Simulizi, Ufahamu, Utungaji, Utumizi wa Lugha na Historia ya Kiswahili.)	90	100%	ziko kawaida

Wakilinganisha mada zingine za isimu wanafunzi 68 sawa na 75.5% katika swali namba 14 walisema mada ya mofimu ni ngumu kuliko mada zingine za isimu. Wanafunzi 22 sawa na 24.5% walisema mada ya mofimu sio ngumu ila kinachosababisha wawe na uelewa mdogo juu ya mada hiyo ni muda mchache wa kujifunza somo la Kiswahili sekondari.

Swala la mtazamo hasi wa mada zilizo ndani ya somo la Kiswahili umewahi kubainishwa na Mbunda (1979) aliybaini kuwa wanafunzi walikuwa na mtazamo hasi wa somo la Kiswahili ndio maana walikuwa hawafanyi vizuri katika mada ya uandishi. Matokeo ya utafiti huo yana uhusiano na utafiti huu kwa kiasi kikubwa

kwa kuwa alichunguza ufundishaji wa mada mojawapo ilijojuishwa ndani ya somo la Kiswahili sekondari, ambapo katika utafiti wa Mbunda na utafiti huu, zote zimeweza kubainisha mtazamo hasi wa wanafunzi na jamii kwa ujumla dhidi ya somo la Kiswahili ambacho kimebeba mada zilizokuwa zinachunguzwa.

Msanjila (2005) katika utafiti wake anasema, inapotokea kuwa shule haina mwalimu wa Kiswahili, mkuu wa shule huweza kuteua mwalimu yejote afundishe somo hilo hatu kama si mwalimu wa somo la Kiswahili. Msanjila anaongeza pia kuonesha jinsi Kiswahili kisivyothaminiwa kwa kutokuwa na semina za mara kwa mara za walimu wa somo hilo na pia kutotengewa fedha nyingi za kununulia vitabu vya Kiswahili na vifaa vya kujifunzia kama yalivyo masomo ya sayansi, Kiingereza na hisabati. Walimu waliojibu swali hili walipendekeza kuwa yafaa hamasa ifanyike kuanzia ngazi ya msingi ili kuleta mtazamo chanya wa somo la Kiswahili hususani mada ya mofimu.

#### **4.6 Hitimisho**

Sura hii imewasilishwa na kuchambua data zilizokusanywa kutoka uwandani. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu na umeongozwa na mkabala wa kimaelezo na wakiidadi. Utafiti ulijikita katika kubaini kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu mofimu tangulizi, mofimu fuatishi na kanuni zinazotawala katika mnyambuliko wa vitenzi vya Kiswahili sanifu. Pia kubainisha sababu zinazopelekea wanafunzi wa sekondari kuwa na kiwango kitakachobainika kwenye lengo namba moja. Imebainika kuwa wanafunzi wa sekondari wanapomaliza kidato cha nne huwa na uelewa mdogo wa mofimu kuhusu mofimu tangulizi, mofimu fuatishi na kanuni zinazotawala

katika mnyambuliko wa vitenzi vyta Kiswahili sanifu. Mwisho utafiti huu ulikusudia kuoanisha mbinu zinazotumika kufundishia na kujifunza mofimu za Kiswahili na kiwango cha ufaulu cha wanafunzi.

## **SURA YA TANO**

### **5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii inahitimisha utafiti unaohusu kiwango cha uelewa wa mofimu tangulizi na mofimu fuatishi na kanuni zinazotawala katika mnyambuliko wa vitenzi vyta Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza inaeleza muhtasari wa utafiti mzima. Sehemu ya pili inatoa matokeo yaliyopatikana katika utafiti na sehemu ya tatu inaeleza mchango wa utafiti. Sehemu ya nne inahusu mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa kuhusu mtaala wa somo la Kiswahili sekondari, muhtasari wa somo la Kiswahili sekondari hususani mpangilio wa mada ulivyo katika muhtasari na mbinu zinazofaa zitumike kufundishia somo la Kiswahili sekondari. Sehemu ya mwisho inapendekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi kutokana na mtafiti alivyobaini umuhimu wa maeneo hayo wakati wa utafiti.

#### **5.2 Muhtasari**

##### **5.2.1 Muhtasari wa Ujumla**

Utafiti huu ulidhamilia kuchunguza mambo makuu matatu. Kwanza, kubaini kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu mofimu tangulizi, mofimu fuatishi na kanuni zinazotawala katika mnyambuliko wa vitenzi vyta Kiswahili sanifu. Pili ni kubainisha sababu zinazopelekea wanafunzi wa sekondari kuwa na kiwango kidogo cha uelewa wa mofimu. Tatu ni kuoanisha mbinu zinazotumika kufundishia na kujifunza mofimu za Kiswahili na kiwango cha ufaulu cha

wanafunzi. Utafiti huu umefanyika katika wilaya ya Uyui, Nzega na Manispaa ya Tabora. Jumla ya watafitiwa 96 walishiriki katika utafiti huu wakiwemo wanafunzi 90 na walimu 6 wa shule za sekondari Idete, Upuge, Imalampaka, Puge, na Uyui iliyoko manispaa ya Tabora.

Data zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya jaribio kama mbinu kuu, mbinu ya pili ni ya mapitio ya nyaraka, kwa mujibu wa utafiti huu insha mbalimbali walizoandika kabla ya utafiti na walizo andika wakati wa utafiti ambamo kulikuwa na matumizi ya mofimu ambazo zimechanaganuliwa kwa mkabala wa kiidadi na wa kimaelezo huku utafiti ukiongozwa na nadharia ya utambuzi ya Benjamin Bloom na wenzake. Nadharia hii ikiwa na lengo la kubaini sababu zinazofanya wanafunzi wa sekondari wanapomaliza elimu ya kidato cha nne huwa na uelewa mdogo wa mada ya mofimu tangulizi na mofimu fuatishi na kanuni mbalimbali zinazotumika katika mchakato wa unyambulishaji wa vitenzi vya maneno ya Kiswahili sanifu.

### **5.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Swali la kwanza la utafiti lililenga kupima kiwango cha uelewa wa mofimu za uambishaji na unyambulishaji wa maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa wanafunzi wanapokuwa kidato cha pili huonekana kama wameielewa mada ya mofimu lakini ufaulu wao huenda unashuka kadiri wanavyopanda kidato cha tatu hadi cha nne. Hali hiyo husababisha wanafunzi kutofanya vizuri kwenye mtihani wa mwisho wa kidato cha nne hususani kwenye maswali ya isimu. Swali la pili la utafiti lililenga kubaini sababu zinazofanya uelewa wa mofimu uambishaji na unyambulishaji wa

maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania utakaodhihirika kwenye swali namba moja. Matokeo ya utafiti yamebainisha sababu mbalimbali zinazosababisha uelewa mdogo wa mofimu kama ifuatavyo: Walimu wasio wazoefu wanaweza wasifundishe vizuri mada za isimu, walimu wa Kiswahili waliowengi hawana uzoefu wa kutosha kufundisha somo la Kiswahili, hivyo kwa kuwa mada za sekondari kwa somo la Kiswahili hujirudia rudia pasipo sababu ya msingi kiasi kwamba mwalimu asiyе mzoefu huweza kiasi cha kushindwa kuwa na uelewa wa mofimu tangulizi na fuatishi zinazotumika katika uundaji wa maneno kwa kutumia mizizi vitenzi vyा Kiswahili sanifu.

Matumizi ya mbinu ya mhadhara ambayo haimshirikishi mwanafunzi katika mchakato mzima wa kujifunza ambapo mwalimu huonekana anajua kila kitu. Wanafunzi wengi wanaosoma shule za kutwa hawapati muda wa kujisomea baada ya muda wa masomo kwa sababu mbalimbali kama vile umbali na majukumu wanayopewa na wazazi/walezi wao wanapofika nyumbani. Wanafunzi wanakosa maarifa yakutosha juu ya stadi mbali mbali za Kiswahili kwa kuwa lugha ya Kiswahili inatumika wakati wa kipindi cha Kiswahili tu, huku masomo mengine yakiendelea kufundishwa kwa lugha ya kiingereza.

Mtaala wa elimu una mapungufu kadha yanayochangia mwanafunzi akose umahiri katika mada tunayoiangalia ya mofimu. Mapungufu haya yameweza kuonekana wakati mtafiti alipokuwa anapitia insha mbali mbali zilizo andikwa na wanafunzi. Matokeo yalionesha kuwa wanafunzi wengi hawawezi kuwianisha maarifa mapya waliyojifunza na maisha yao ya kila siku. Wanafunzi wachache tu ndio walioweza kuwianisha maarifa mapya waliyojifunza na maisha ya kila siku. Walimu walisema

mtaala una mapungufu sababu mtaala tulionao hautoi fursa kwa mwalimu awe mbunifu, mtaala unamtaka ajikite kwenye maudhui ya mada husika yaliyopangwa na wizara ya elimu, hivyo mwalimu analazimika kuwa mtumwa wa mtaala na silabasi ya Kiswahili.

Mtiririko wa mada kwenye muhtasari zilivyopangwa haukuzingatia kiwango cha uelewa na umri wa mwanafunzi. Walimu waliohojiwa waliendelea kusema kuwa, mada zilivyopangwa kwenye muhtasari haziendi sanjari na utaratibu wa uwasilishaji wa maarifa mapya kwa mwanafunzi, utaratibu unamtaka mwalimu anapofundisha aanze kufundisha vitu rahisi kwenda vigumu. Hali hii haijazingatiwa katika upangaji wa mada kwenye silabasi.

### **5.3 Hitimisho**

Utafiti huu ulipima kiwango cha uelewa wa mofimu za uambishaji na unyambulishaji wa maneno ya Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania. Katika uchunguzi wetu na jinsi data zilivyodhirisha, tunaweza kuhitimisha yafuatayo:

Mbinu ya mhadhara inayotumiwa na walimu wa sekondari kufundishia Kiswahili inachangia kwa kiasi kikubwa wanafunzi kutokuwa na uelewa wa mofimu. Lugha ya Kiingereza kuendelea kutumika kufundishia na katika mawasiliano ya kawaida katika shule za sekondari inachangia Kiswahili kutokupewa nafasi sawa ya kutumika shuleni kama ilivyo kwa Kiingereza. Wanafunzi wanaosoma shule za kutwa hawapati muda wa kujisomea wanapokuwa nyumbani baada ya muda wa masomo na zile siku za mapumziko. Mtaala wa somo la Kiswahili sekondari una mapungufu yanayohitaji marekebisho.

## **5.4 Mapendekezo**

### **5.4.1 Mapendekezo ya Kiutekelezaji**

Mtafiti anapendekeza yafuatayo kwa mamlaka zinazohusika kutokana na data ziliyochanganuliwa:

Baraza la mitihani la Tanzania lisawazishe alama katika mada zote za somo la Kiswahili sekondari ili kuondo tatizo la alama nyingi kuelemea upande wa fasihi.

Wanafunzi wajengwe kisaikolojia ili wawe na mielekeo chanya dhidi ya mada za isimu. Pendekezo la pili hapo juu litawezekana kama ikiwa kutakuwa na walimu wanaofundisha isimu pekee sekondari, hivyo kuwe na walimu wa isimu kuanzia ngazi ya sekondari.

Vitabu nya kiada vinavyokinzana vibainishwe na kurekebishwa.

Walimu wa sekondari wanapokuwa chuoni na kwenye mafunzo anuai ya kuwaongezea ujuzi wafundishwe namna bora ya kutumia njia shirikishi ya kufundishia na kujifunzia. Uhamishaji wa walimu wa sanaa kutoka sekondari kwenda shule za msingi ufanywe kwa kuzingatia umahiri wa mwalimu tofauti na sasa unafanywa kwa kuangalia wingi wa walimu waliopo kituoni bila kujari mahitaji ya halisi ya walimu wa isimu na fasihi waliopo kituoni. Baraza la mitihani wawe na kanzi data ya walimu mahiri wa isimu walioko shule za msingi na sekondari ili wawatumie katika usahihishaji wa mitihani ya kidato cha pili na cha nne.

### **5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti Fuatishi**

Utafiti huu umepima kiwango cha uelewa wa mofimu tangulizi na fuatishi katika mizizi ya vitenzi nya Kiswahili sanaifu kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania.

Mtafiti anapendekeza maeneo yafuatayo yafanyiwe utafiti:

Kuchunguza iwapo kuna haja ya kuwa na kitabu rasmi cha mada za isimu pekee kwa shule za sekondari nchini. Kutathmini sababu za wanafunzi kuwa na ufaulu duni wa mofimu ikilinganishwa na vipengee vingine vya isimu ya Kiswahili. Kuchunguza ubobezi wa waalimu wa Kiswahili kuhusu Mofimu. Kufanya utafiti linganishi wa ufahamu wa Mofimu kwa wanafunzi waliopitia mtaala wa Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika elimu ya msingi na wale walioptia mtaala wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia.

Tafiti zilizopendekezwa katika sehemu hii zikitekelezwa pamoja na utafiti huu zitakuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza taaluma ya isimu hususani katika kipengele cha mofimu.

## MAREJEREO

- Abudulla, S.H.(2016). *Viambishi njeo katika vitenzi vya lahaja ya Kipemba: Uchanganuzi wa kimofofonolojia kuonesha muundo ndani na muundo nje.* Tasnifu za Uzamili.Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar: Including Innotation.* London: Longmans
- Besha, R.M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Criper C. na Dodd N. (1984). *Report on the Teaching of English Language and its Use as a Medium in Education.* Dar es Salaam, Mimeo.
- Crystal, D. (1991) *A Dictionary of Linguistics and Phonetics.* New York: Bluckid Publishers.
- Gawasike A. (2011). *Unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya kibantu.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Habwe, J na Karanja, P (2004), *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili,* Nairobi, Phoenix
- Haki Elimu (2014). *Ufanisi katika Ufundishaji kwenye Shule za Msingi na Sekondari nchini Tanzania.* Dar es Salaam,
- Hassan, S.H. (2016). *Ujidhirishaji wa Mofu Nafsi na Njeo Katika Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Haule, F. (2014). *Muundo wa Njeo za Lugha ya Kingoni.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.
- Hornby, A.S. (2006) *Oxford Advanced Learner's Dictionary of Current English,* Oxford University Press, UK, 1435 pp

*Hooper.J (1976) .Introduction to Genative Phonology, London: Oxford University press.*

J.A.Masebo; Nyambari Nyangwine (2002)*Swahili languageGrammar*.Dar es Salaam, Tanzania: The General Booksellers Ltd.

Kahigi, K. K (2009), *Unyambulishaji wa Nomino na Kitende kati Kikahe*, katika *KISWAHILI*: Jarida la Uchunguzi wa Kiswahili. JUZUU 5. Dar es Salaam, TUKI

Kahn, D. (1976). *Syllable – Based Generalization in English Phonology*. PhD Dissertation, MIT. (Published by Garland, 1980).

Katamba, F. (1989). *An Introduction to Phonology*. New York: Longman Publishers.

Katamba, F. (1993). *Modern Linguistics: Morphology*. New York: Palgrave Publishers. Khamis, A. M (1985), *Swahili Verb Derivation*, Unpublished Ph. D Dissertation, University of Hawaii

Khamis, A. M (2008), *Maendeleo ya Uhusika*, Chuo Kikuu cha Dar es Saam, TUKI.

Khamis, A. M (2009), *Stadi za Lughya ya Kiswahili: Sarufi I*, Dar es Salaam, TUKI

Kiango, J. G (2008). *Sura ya Vinyambuo Vitenzi vya Kiswahili: Mtazamo mbalimbali kuhusu kanuni za unyambuaji, katika Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lughya za Kiafrika*, ukurasa 45-58. Nairobi, Moi University Press

Kihore, Y. M. (2009). *Stadi za Lughya ya Kiswahili sanifu*, Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Kihore, Y. M. (2001), *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA)*.Sekondari na Vyuo. Dar es salaam:Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Kihore, Y. M (2003), *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA)*. Dar es salaam: TUKI.

Kipacha, A. (2007). *Lahaja za Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo kikuu Huria cha Tanzania. Kiputiputi, O.M.(2001). “*Ufundishaji Sayansi kwa Kiswahili.Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili 2000*”. Imehaririwa na J.S. Mdee na H.J.M. Mwansoko, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili na Chuo Kikuu cha Dar es salaam.Uk 350-373.

Kombo D.K. and Tromp D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing;Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C. K. (1990).*Research Methodology;Methods and Techniques*; New Delhi: New Age International (p) Limited.

Kothari, C. K. (1993). *Methodology: Methods and Techniques*. New Delh: Wiley Enstern Ltd. Kothari, C. R. (2004) *Research methodology Methods and Technique (Second Revised Edition)*.New Delhi: New age International Publishers

Kothari, R. C. (2008), *Research Methodology; Methods*. New Delhi New Age International Publishing LTD Techniques.

Leedy, P.D. (1980). *Practical Research: Planing and Design*. New York: Macmillan Publishing Company Limited.

Mashaka, W. (2015). *Athari za Lughya ya Kijita katika Kujifunza Kiswahili*;Tasinifu ya Uzamili,Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D.P.B. (2004) *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA)*. Sekondari na Vyuo. Dar es salaam:TUKI.

Massamba, D. P. B (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lughya*. Chuo kikuu cha

- Dar-es-Salaam: TUKI. Massamba na wenzake. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.
- Massamba, D. P. B. (2002, *Historia ya Kiswahili*. Nairobi : Jomo Kenyatta Foundation.
- Massamba, D. P. B. (2004), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*, Dar es salaam: TUKI Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2008), *NADHARIA YA LUGHA.KISWAHILI 1. Kidato cha 5 Na 6.Nyambari* Nyangwine Publishers.Dar es salaam
- Matei, A. K (2008), *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi*, Nairobi, Phoenix Publishers
- Matinde, R. S, (2012), *Dafina ya Lugha: Isimu Nadharia kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na VyuoVikuu*.Dare es salaam” Serengeti Educational Publishers (T) Ltd. Mdee, J.S. (2001). Makala ya kongamano ya Kitaifa, TUKI, Dar es salaam.
- Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi : Longhom Publishers.
- Mlama P. na Materru M. (1978). *Haja ya Kutumia Kiswahili katika Kufundishia Elimu ya Juu*. Lugha Yetu 35 Dar es Salaam, BAKITA
- Mligo, E.S. (2012). *Jifunze Utafiti Mwongozo kuhusu utafiti na Utamaduni wa Ripoti yenye Mantiki*.Dar es salaam:Ecumenical Gathering (EGYS).
- Mkude D.J. (1982).*Matching education with communicative skills in Kiswahili*.In H.R TRAPPES-LOMAX, R.M. BESHA and Y.Y. MCHA (eds) *Changing Language Media*. Univrsity of Dar es Salaam.
- Mohammed, M. A. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: Sitima Printers &

- Stationers Ltd. Msanjila, P.Y. (2004). *Isimu Jamii*. Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).
- Mugenda, O. M. & Mugenda, A. G. (2003). Research methods: Quantitative and qualitative Approaches. Nairobi: African Centre for Technology Studies.
- Nyanda J. (2015). *Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Nyandago, F.O. (2013). *Uchanganuzi Linganishi wa Sintaksia ya Sentensi sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Oichoe, M.P. (2005) *Ulinganishi wa Kirai Tenzi cha Kiswahili Sanifu na Ekegusii Kimofosintaksia; Mtazamo wa Uminimalisti*. Tasinifu ya M A.Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Omary, M. (2010;2011). *Siasa katika Ushairi wa kezilahabi*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Orodho, J. A. (2009). *Elements of Education and Science Research Methods*. 2ed. Maseno: Kanezja Publisher.
- Ouhalla, J. (2006). *Introducing Transformational Grammar. From Principles and Parameter to Minimalism*. 2 ed. London: Arnold Publishers.
- Polome, E. C (1967). *Kiswahili Language Handbook*, Washington D.C, Center for Applied Linguistics
- Ruane, J.M. (2005) *Essentials of Research Methods: A Guide to Social Science Research*. Blackwell Publishing, Hoboken.
- Rubanza, Y. I (1988), *Linear Order in Haya Verbal Morphology: Theoretical Implication*, Unpublished Ph.D. Dissertation, Michigan State University

- Rubanza, Y. I (1996), *Mofolojia ya Kiswahili*, Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
- Qorro, Martha (1997).*The Role and Place of Language in Education and Society*:The Case of Kiswahili and English in Tanzania.Papers in Education and Development 18:129-144.
- Richards, J.C. (1972). *Social Factors, Inter Language and Language Learning* 22:159-188.
- Ryanga, O.W.A. (2007). *Dhana, Mbinu za Utafiti na Utendakazi wake*. Nairobi: Kenyata University.
- Roy-Campbell & Qorro M. (1987).*A survey of the Reading Competence in English of Secondary School Student in Tanzania*. Dar es Salaam; University of Dar es saalam.
- Rubangumya, CM. (1990). *Language in Education in Africa: A Tanzanian Perspective Clevadon Multilingual Matters*. University of Dar es salaam.
- Rubangumya, C.M. (1996). *What Research tells us about Language of Instruction in Tanzania*.Nairobi:IDRC.
- Selinker, L. (1972). Interlanguage. *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching*, 10(3), 219-231.
- TUKI, (1990), *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lughu*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
- TUKI TUKI, (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press & TUKI .Uwezo, (2011). *Are our Children Learning?Annual Learning Assessment Report* Dar es salaam.Uwezo Tanzania.

Vuzo, M.S.(2002) *Pedagogocal Implications of using English as Language of Instruction in Secondary Schools in Tanzania\_Report No9 Education in Africa .Vol.11* Oslo;Institute of Educational Research.

Waihiga, G (1999), *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*, Nairobi, Longhorn Publisher  
Wamitira, K, W, (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*, Nairobi: English Press.

Williman, N. (2011) *Research Methods; The Basic*, London and New York:  
Routledge Taylor and Francis Group. Wizara ya Elimu na Utamaduni,  
(1996).*Muhtasari wa Kiswahili*. Dar es Salaam. Wizara ya Elimu na  
mafunzo ya ufundi (2010) *Mhtasari wa Kiswahili Sekondari kidato cha I-IV*.

## KIAMBATISHO Na 01

Maswali ya Jaribio

Jina .....

Jinsia .....

Kidato cha .....

Maswali ya wanafunzi

1. Mizizi ya vitenzi vyenye irabu /a/, /i/ na /u/ hutumia mofimu gani katika kuwakilisha mofimu ya kutendesha? (a) – ish- (b) – esh- (c) – ek- [ ]
2. Unafikiri ipo tofauti kati ya mofimu na viambishi NDIYO / HAPANA .....
3. Lugha ya Kiswahili ina alomofu mbili tu za utendea nazo ni / / na / /
4. Kwa kutumia mifano, eleza maana na aina ya mofimu
5. Kwa kutumia mifano eleza dhima ya mofimu katika uundaji wa maneno ya lugha inayohusika.
6. Eleza tofauti kati ya viambishi awali na viambishi tamati.
7. Eleza tofauti iliyopo baina ya mzizi na shina katika vitenzi vyta Kiswahili.
8. Fafanua maana na aina ya viambishi katika lugha ya Kiswahili.
9. Onyesha mofimu zilizomo katika maneno yafuatayo na eleza kazi za kila mofimu:
  - (i) hawajaonana
  - (ii) kilichonunuliwa
  - (iii) anasimama
  - (iv) Ukiniletea
  - (v) Hatukuwatafuta
  - (vi) Ondoana
10. Mada ya mofimu ni nyepesi na inaeleweka vizuri kwa wanafunzi  
NDIYO / HAPANA
11. Mada ya mofimu ni nyepesi na inaeleweka vizuri kwa wanafunzi kidato cha pili  
NDIYO / HAPANA
12. Unafikiri ipo tofauti kati ya mofimu na viambishi NDIYO / HAPANA .....

13. Je, huwa unapata muda wa kujisomea unapokuwa nyumbani baada ya kutoka shuleni?
14. Je, kuendelea kutumika kwa lugha ya kiingereza kwa shule za sekondari kama lugha ya kufundishia na mawasiliano ya kawaida kunachangia kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mofimu?

## KIAMBATISHO Na 02

Maswali ya insha kwa wanafunzi

Bainisha matumizi ya mofimu za njeo, hali, ngeli, aina za viambishi na mofimu za utendea katika hotuba ifuatayo:

“ Waziri wa kilimo, Mkuu wa Wilaya, mwenyekiti wa Kijiji, wanachama wa kikundi cha JUHUDI, mabibi na mabwana. Ni matumaii yangu kwamba nyote mu buheri wa afya. Mimi ni mwakilishi wa Kikundi cha Mshipi wa Kijani Kibichi, na jioni ya leo na washukuru sana tumekutana tuzungumze mambo kadhaa ya takayo tufanya tuweze kuboresha mazingira yetu.”

Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa:

Panga – tendea, tendwa, tendewa a tendeka

Taga – tendwa, tendeka, tendana na tendesha

Hama – tendea,tendana,tendeana na tendwa

Chukua – tendeka,tendesha,tendea na tendewa

Twa – tendea, tendewa,tendwa na tendesha

3.Ainisha viambishi tangulizi,fuatishi na njeo vinavyojitokeza kwenye mazungumzo baina ya mwalimu Mkuu, mzazi na mwanafunzi juu ya nidhamu ya mwanafunzi huyo:

Mwalimu: - Bwana Juma nimekwita umuchukue mtoto wako ukamsomeshe katika shule nyingine kwa kuwa sisi ametushinda.

Mzazi: - Ikiwa amewashinda na ninyi ndio mlion na kiboko, si ataniua mimi!! Hata mimi simtaki kwa maana simwezi, hawezi kuja kangu

Juma –nimesema Mimi sitaki kusoma nimechoshwa na mtindo huu wa viboko.

*KIAMBATISHO Na 03*

Maswali kwa walimu wa Kiswahili

Jina .....

Umri .....

Jinsia .....

Kiwango cha elimu .....

**MASWALI**

1.Kuna tofauti yoyote unayoipata unapofundisha mada ya mofimu kwa kidato cha pili na unapofundisha mada hiyo hiyo kwa wanafunzi wa kidato cha nne

(A) Uelewa wa wanafunzi wa kidato cha pili uko juu

(B) Uelewa wa wanafunzi wa kidato cha nne uko juu

(C) Uelewa upon sawa kwa wanafunzi wa kidato cha NNE na kidato cha pili

(D) Inategemea na aina ya mwalimu [ ]

2.Je,ni mbinu zipi unazotumia kufundisha mada ya mofimu kidato cha pili

(A) majadiliano katika vikundi

(B) maswali na majibu

(C) zote A na B [ ]

3. Je, kuna uwiano wowote kati ya mbinu zinazotumika kufundishia na kiwango cha uelewa wa wanafunzi?

4.Toa maoni yako juu ya ufundishaji wa mada ya mofimu inayofundishwa kidato cha pili.....  
.....  
.....

5. Unafikiri kunatofauti kati ya mofimu na viambishi, toa mifano mbalimbali ya kuonesha kama kuna tofauti au hakuna tofauti.
6. Taja matatizo yaliyomo katika mtaala wa sekondari Tanzania yanayoathiri ujifunzaji wa mada ya mofimu.
- (i).....
- (ii).....
- (iii).....

#### KIAMBATISHO NA 04

#### **BAJETI YA TASNIFU 2018**

NO	UCHAPAJI WA KAZI	GHARAMA
1.	Kununua za tarakirishi	460,000/=
2.	Kuchapisha pendekozo nakala ya kwanza	6,000/=
3.	Kuchapa maerekebisho ya pili ya pendekozo	7,500/=
4.	Kuchapisha ripoti ya mwisho ya pendekozo	8,000/=
5.	Kuchapisha hojaji	12,000/=
6.	Vifaa vya kuandikia (kalamu,karatasi)	13,000/=
7.	Usafiri wakati wa kukusanya kusambaza hojaji na kukusanya data.	35,000/=
8.	Kuunganisha ripoti ya mwisho ya tasnifu,nakala tatu za tasnifu.	90,000/=
	Jumla kuu	699500/=

*KIAMBATISHO NA 05*

## RATIBA YA WAKATI

KAZI	SPT- 2017	OCT- NOV 2017	NOV- DES 2017	JAN 2018	FEB- APRL 2018	MEI – AUG UST 2018	SEPT 2018	SEPT 2018
Mada iliyotolewa kwa wakati	XXX							
Utafiti kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada		XXX						
Kuandika pendekozo la utafiti			XXX					
Kuwasilisha pendekozo la utafiti kwa msimamizi				XXX				
Kukusanya data				XXX	XXX	XXX		
Kuwasilisha na kuchanganua data						XXX		
Kuwasilisha mswaada wa kwanza wa tasnifu						XXX		

Marekebisho ya mswada						xxx		
Kuwasilisha nakala tatu za tasnifu kwa msimamizi							XXX	
Utetezi wa tasnifu								XXX

KIAMBATISHO NA. 6  
 THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

*FACULT OF ARTS AND SOCIAL SCIENCES*

P.O. Box 23409



Tel: 255-22-2666752/2668445  
 ext.2101

Fax: 255-22-2668759

DIRECTOR,

DRPS,

THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA,

P.O. BOX 23409,

DAR ES SALAAM

Dear Sir,

Re: CLEARANCE TO CONDUCT RESEARCH WORK FOR MR. NDALAHWA BNZALI

This is to inform you that, Mr. NDALAHWA BNZALI is an MA student under my supervision.

Title of the research proposal: **KUPIMA KIWANGO CHA ULEWA WA MOFIMU ZA UAMBISHAJI NA UNYAMBULISHAJI WA MANENO YA KISWAHILI SANIFU KWA WANAFUNZI WA SEKONDARI TANZANIA**

Registration No: PG201609981

I am writing to certify that, the student has incorporated all the comments I have been giving him to my satisfaction.

I therefore, recommend him to you to be granted research clearance for data collection in the field from 01 December to 30 April, 2018. The field will be done in Uyui District, Nzega District and Tabora Municipal. The letter is to be addressed to District Education Officers. respectively.

Thank you in advance.

Sincerely,

Dr. Zelda Elisifa Sam

S/ Lecturer in Linguistics and Literary Studies

Supervisor

**KIAMBATISHO**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
 PRESIDENT'S OFFICE  
 REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT  
 TABORA MUNICIPAL COUNCIL

(All correspondence should be forwarded to the Municipal Director)

TABORA REGION  
 TEL: 026 2604315/6088



MUNICIPAL DIRECTORS' OFFICE  
 P.O. BOX 174 – TABORA.

Ref.No. TMC/ESC/IID/235

Date: 20/03/2018

Uyui Secondary School,  
 Itonjanda Secondary School  
**TABORA MUNICIPALITY.**

**RE: REQUEST FOR UNDERTAKING RESEARCH.**

Please refer to heading above.

I am pleased to inform you that **Mr. Ndalahwa Bunzali** who is a student from **Open University of Tanzania** has requested to conduct his research at your school. His research topic is: **Kupima Kiwango cha Uelewa wa Mofimu Awali na Mofimu Tamati na Myambuliko wa Vitenzi vyta Kiswahili Sanifu kwa Wanafunzi wa Sekondari Tanzania: A Case of Tabora Municipality.** Hence, kindly you are asked to host the mentioned person for further procedures once he reports at your school. Your school will not be responsible to offer any kind of payment concerning his field work.

*Sitta P. Ndamayape*  
 For: MUNICIPAL SECONDARY EDUCATION OFFICER  
 TABORA

MUNICIPAL SEC. EDUCATION OFFICER  
 P. O. BOX 174  
 TABORA

*Ogoda*  
 SENIOR ACADEMIC MASTER  
 UYUI SECONDARY SCHOOL  
 TABORA  
 11/04/2018

*MAKAMU MKUU WA SHULE*  
 ITONJANDA SEKONDARI  
 TABORA  
 11/04/2018

## KIAMBATISHO:

### HALMASHAURI YA WILAYA YA TABORA

(Barua zote zilumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji(W)

SIMU : +255 (26) 4351  
FAX : +255 (26) 4351

Unapojibu tafadhalu nukuu:



S.L.P. 610,  
TABORA.

Kumb. Na. WHT/EL/SG/04/26

21 /3/ 2018

Wakuu wa Shule,  
Shule za Sekondari, Idefe, Imalampaka na Upuge.

**YAH: KUMTAMBULISHA MWALIMU NDALAWA BUNZALI KWA AJILI YA UTAFITI**

Kichwa cha barua chahusika.

Namlela kwenu mwalimu mtajwa hapa juu ambaye anafanya utafiti kwa hatua ya ukusanya data kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (The Open University of Tanzania) katika mada ya **KUPIMA KIWANGO CHA ULEWA WA MOFIMU ZA UAMBISHAJI NA UNYAMBULISHAJI WA MANENO YA KISWAHILI SANIFU KWA WANAFUNZI WA SEKONDARI TANZANIA**.

Mwalimu huu anasoma shahada ya Umahirri katika kozi ya MA- Kiswahili.

Naomba apewe ushirikiano katika kufanikisha zoezi hilo.

Nawatakieni kazi njema.

*Amos B Wigayi*

Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W)  
TABORA

*Paul John Mdalisi*  
Mkuu wa Shule Idefe Sek.  
22.03.2018

**MKUU WA SHULE  
SHULE YA SEKONDARI IDEFE  
S. L. P 640, TABORA**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR

TABORA

*Noah NK*, Afifica kuku zenge data.

*Malampaka Sekondari*  
**MKUU WA SHULE**  
SHULE YA SEKONDARI MALAMPAKA  
IYUI - TABORA

*John H. H.*  
Kr y MKUU WA SHULE  
UPUGE SEKONDARI  
UYUITABORA  
09.04.2018

## JEDWALI LINALOONESHA MAENEKO YALIYOFANYIWA MAREKEBISHO

22/10/2019

UKURASA	SURA	MAKOSA	KOSA LILIVYOSHUGHULIKIWA
IV	IKISIRI	Zinavyopelekea	Neno linalotumika sasa ni[zinazofanya] kama ilivyoshauliwa.
xiv	Orodha ya vifupisho	KT-Kirai Tenzi	Kitenzi
Uk. 1	Sura ya kwanza	Yaani,(sz), Kiswahili kama lugha ya pili,hapo juu	Maeneo yote hayo yameondolewa kama ilivyoshauliwa.
Uk.1		Aina za mofimu za utafiti huu zitajwe bila kubadilika badilika taz.1.3.1, 1.3.2,1.5	Aina za mofimu zimerekebishwa katika maeneo yaliyotajwa ambapo yametumika maneno mawili tu, kiambishi awali na kiambishi fuatishi kwa maana ya kiambishi tamati.
Uk.2		Ujifunzaji wa lugha za kiafrika katika muktadha wa matumizi yake kama lugha ya	Ujifunzaji wa lugha za kiafrika katika muktadha wa matumizi yake kama lugha ya kufundishia kwa kiasi kikubwa zimefanywa

		kufundishia kwa kiasi kikubwa sana na watafiti wa nje	ndani na nje ya Tanzania
Uk.3		Hata hivyo kumekuwa na malalamiko?	Hata hivyo kumekuwa na malalamiko ya walimu wanaofundisha somo hilo
Uk.4		Unaonesha viwango vya ufaulu wa somo la Kiswahili,	Unaonesha kuwa viwango vy ufaulu wa somo la Kiswahili uko chini
		Matokeo ya utafiti yanaonesha somo la Kiswahili ufaulu wake uko chini hususani kwa shule za vijijini	Sentensi hii imetolewa ili kuleta mtiririko mzuri wa mawazo
Uk.5		Lengo namba moja	Lengo mahsus no.1 limeongezwa maneno (kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania}
Uk.6		Mawanda ya utafiti	Mawanda ya utafiti yamebadilishwa na kuandikwa malengo mahsus ya utafiti huu , pia kwenye ufanuzi wa kundi lengwa zimeongezwa shule sita

			zilizofanyiwa utafiti kwani kulikuwa na idadi tu ya shule.
Uk.6		Changamoto	Changamoto hoja ya kwanza imetolewa na kubaki hoja namba mbili ya matumizi ya mbinu ya dododso kwani hoja iliyoondolewa haikuwa changamoto.
Uk.9	Sura ya pili	Atakayejifunza Kiswahili akiwa Tanzania [sentensi ilikuwa haileti maana iliyokusudiwa.	Sentensi itasomeka [atakayejifunza Kiswahili akiwa Tanzania kwa kuwa atakuwa anaishi na jamii inayotumia lughya ya Kiswahili]
Uk 16		Sehemu ya hitimisho	Imeongezwa maneno [sura inayofuata inahu mbinu za utafiti]
Uk. 17	Sura ya tatu	3.3 Eneo la utafiti	Maneno yafuatayo yameongezwa [Utafiti huu ulifanyika katika wila ya tatu Nzega, Uyui, na manispaa ya Tabora]
Uk. 18		3.4 Kundu lengwa idadi ya shule zimetajwa 8	Shule zilizofanyiwa utafiti ni sita

Uk.19		3.5 maneno sampuli na usampulishaji	Neno usampulishaji limetumika likiwa na maana ya mchakato ewa ekuchagua sampuli na sio aina ya njia iliyotumika katika usampulishaji
Uk.23		3.7.2 Mbinu ya 3mapitio ya nyaraka	Imesomeka mapitio ya insha
Uk.28		Hitimisho inasema watafitiwa walikuwa 120	Jumla ya Wanafunzi walikuwa 90
Uk.30	Sura ya nne	4.2.2 idadi ya wanafunzi aya ya mwisho	Aya hiyo imeondolewa kwa haihusiani na mada
Uk.35		Jedwali namba 4.4 viambishi unyambulishi	Imekuwa viambishi vy a unyambulishaji
Uk.41		4.5 Sababu zinazosababisha wanafunzi kuwa na uelewa mdogo	Inasmeka [mambo yanayosababisha
Uk.42		Aya ya pili ilikuwa na italiki	Italiki imeondolewa
Uk.43		Mbinu ya ushuhudiaji	Mbinu hii imeondolewa kwa

			kuwa haipo katika sura ya tatu
Uk. 52		4.54 Mapungufu ya mtaala aya ya mwisho orodha ya waandishi haikupangwa kwa miaka	Waandishi wamepangwa kwa miaka
Uk. 56	Sura ya tano	Baraza la mitihani wawe na kanzi data ya walimu mahiri wa isimu walioko shule za msingi na sekondari ili wawatumie katika usahihishaji wa mitihani ya kidato cha pili na cha nne.	Pendekezo hili limeondolewa kama ilivyoshauriwa kwani tafsiri yake inalenga kubeza walimu wanaofundisha shule za sekondari kuwa hawana maarifa ya kutosha.
Uk. I-63	Sura ya kwanza mpaka ya tano	Maeneo mengi yalihitaji kufanyiwa uhariri kabla ya kazi haijakusanywa	Kazi yote imehaririwa kuanzia sura ya kwanza mpaka ya tano. Mfano, taratibu za kiuandishi zilikuwa hazikufuatwa kama vile matumizi ya herufi kubwa na ndogo, nafasi kati ya neno na neno au silabi na silabi nk.